# Nipashe

Jumamosi Aprili 17, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580553

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US



**Ndugai** asema uaminifu kwa vijana washuka

UKURASA 2



**Wabunge** wanaotumia usafiri wa bodaboda wapewa tahadhari

UKURASA 7

**Pogba asaini dili na Amazon Prime**

UKURASA 21

# Mwanga wa matumaini



• **Ni** kuhusu kikokotoo mafao ya wafanyakazi ukomo wa utumishi... *Endelea ukurasa 2*



Dk. Edward Hosea (wa pili kushoto), akishangilia na mashabiki wake baada ya kuibuka mshindi wa urais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) katika uchaguzi mkuu wa 2021, uliofanyika jijini Arusha jana. **Picha ndogo:** Wanachama wakipiga kura katika uchaguzi huo. **PICHA ZOTE: GETRUDE MPEZYA**



## Wastaafu 6,800 waweka mafao bil. 1/- kibindoni

UK. 2

## Hoseah aibuka mshindi urais TLS

UKURASA 3

**MICHEZO** **YANGA, BIASHARA MECHI YA KIBABE** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Wastaafu 6,800 waweka mafao bil. 1/- kibindoni

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, amesema serikali imetoa Sh. bilioni moja kwa ajili ya kuwalipa wastaafu 6,793 wa Mfuko wa Jamii wa Watumishi wa Umma (PSSSF).

Alitoa ufafanuzi huo jana bungeni, kufuatia mchango uliotolewa na Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Halima Mdee, kudai kuwa serikali inadaiwa fedha nyingi na wastaafu nchini.

Kwenye hoja yake, Mdee alitaka serikali kulipa deni inalodaiwa katika mifuko ya hifadhi ya jamii ili iweze kuwa endelevu na wastaafu walipwe kwa wakati.

Alisema katika Ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali (CAG), madeni ya ndani ambayo serikali inadaiwa ni Sh.trilioni 2.7 lakini kuna fedha zingine Sh.trilioni 7.1 ambazo PSSSF ilipewa jukumu la kulipa wastaafu ambao wamekidhi vigezo vya kulipwa lakini hawajachangiwa.

Mdee alihoji zaidi ni kwanini serikali isitenge Sh. trilioni moja kila mwaka kulipa mifuko na kwamba kuna madeni ambayo yameiva tangu mwaka 2017, lakini imekuwa ikitolewa ahadi ambayo haitekelezwi na kusababisha wastaafu kusubiri mafao yao kwa muda mrefu na wengine kufariki bila kupata.

Akijibu hoja ya Mdee, Waziri Mhagama alisema kwa sasa serikali imeanza kufanya tathmini ili kupata taarifa sahihi ya hali halisi ya mifuko iliyopo na nini kifanyike kuboresha sekta hiyo.

"Kwa hali ya haraka tu wastaafu wa PSSSF 132,670 wamelipwa mafao na tunabaki na madeni ya nyuma ya wastaafu 6,793 ambao tunaendelea nao na juzi Hazina wametupa Sh. bilioni moja ili kuwalipa hawa waliobaki, matatizo yapo lakini serikali inatafuta suluhu katika kuyatatua,"alisema Mhagama.

Pamoja na hayo, Waziri Mhagama alisema thamani ya mifuko yote ya hifadhi ya jamii imefikia Sh.trilioni 11.51 na imeendelea kuongezeka.

Alisema: "Baada ya kupata ripoti ya tathmini tunayoifanya ya mifuko ninawahakikisha serikali itakuwa imejipanga kumaliza matatizo ya mifuko hii na hasa PSSSF ambao tunataka kuupa kikokotoo ambacho kitakuwa himilivu kwa faida ya wanachama na uhimilivu na uendelevu wa mfuko, itatusaidia kupata uamuzi endelevu".

Wakati huo huo, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Watu Wenye ulemavu, Ummy Nderiananga, alisema hadi Januari mwaka huu, wamewatambua watoto wenye ulemavu 28,698 na kuandikishwa shuleni.

Alisema serikali itaendelea kusimamia eneo la ajira watu wenye ulemavu na kutoa wito kwa waajiri kuendelea kuwaamini kwa kuwa uwezo wanao.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akizungumza wakati akihitimisha hoja ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Taasisi zake na Ofisi ya Bunge, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Serikali yaunda kamati kikokotoo cha mafao

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

SERIKALI imeunda kamati mahususi kushughulikia dosari zilizojitokeza katika kanuni mpya za ulipaji mafao ya wastaafu, Nipashe imepewa taarifa.

Uamuzi huo umechukulia ukiwa umebaki mwaka mmoja kabla ya kuanza kutumika kwa kikokotoo kipya katika ulipaji wa mafao ya wastaafu, ambacho kwa mujibu wa kanuni, kimeweka utaratibu wa kulipa mafao kwa mkupuo kwa asilimia 25 na asilimia 75 inayobaki kulipwa kama mshahara kwa mstaafu kwa miaka 12.5.

Katika mazungumzo maalum na Nipashe kwenye Viwanja vya Bunge jijini Dodoma jana, Waziri Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, aliweka wazi kuundwa kwa kamati hiyo.

"Serikali imeunda kamati maalum ya kushughulikia hilo suala la kanuni ya ulipaji wa mafao kwa watumishi. Siwezi kuweka wazi kinachoendelea kwa sababu hawajamaliza kazi.

"Mtafute Katibu Mkuu atakupa taarifa za kina zaidi walipofikia kwa sasa, lakini ninachojua kamati ile inaendelea na kazi tuliyowapa," alisema. Nipashe ilimtafuta Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Tixon Nzunda, ambaye alikiri kuundwa kwa kamati hiyo.

Hata hivyo, Nzunda hakuwa tayari kubainisha hatua iliyofikiwa na kamati hiyo katika kushughulikia dosari zilizojitokeza katika kanuni mpya za ulipaji wa mafao, akisisitiza kamati ipewe muda wa kufanya kazi iliyotumwa.

"Ni kweli kuna kamati imeundwa na serikali kushughulikia suala hilo, mpaka sasa wanaendelea kulifanyia kazi kwa kushirikisha wadau kwa maana ya vyama vya wafanyakazi.

"Watakapokamilisha kazi, tutaujulisha umma kilichoafikiwa, hivyo kuweni na subira, tuipe muda kamati ifanyie kazi suala hilo. Karibu sana wizarani kwetu," alisema.

Jumanne wiki hii, wakati akiwasilisha bungeni hotuba yake kuhusu mwelekezo wa kazi za serikali na makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi yake kwa mwaka ujao wa fedha, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema serikali itashirikiana na wadau kupata kanuni za ulipaji wa mafao hayo zitakazokidhi matarajio ya wafanyakazi. "Katika mwaka 2021/22, serikali kwa kushirikiana na wadau wengine, itaendelea kusimamia utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Rais ili kuwezesha kupata kanuni za ulipaji wa mafao ambazo zinakidhi matarajio ya wafanyakazi wa sekta ya umma na binafsi," alisema Majaliwa.

Oktoba 20, 2017, Bunge lilipitisha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ambayo mbali na kuunganisha mifuko ya pensheni kuunda Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) na kufanya marekebisho kwenye Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF), kanuni zake ziliweka utaratibu wa kulipa mafao kwa mkupuo kwa asilimia 25 na asilimia 75 inayobaki kulipwa kama mshahara kwa mstaafu kwa miaka 12.5.

Sheria hiyo ambayo pia iliweka umri wa kustaafu kuwa miaka 55 kwa hiari na miaka 60 kwa lazima (kwa kada maalum kama vile madaktari na maprofesa umri wa kustaafu ni miaka 60 kwa hiari na miaka 65 kwa lazima), iliibua mjadala mkali kitaifa uliosababisha aliyekuwa Rais kipindi hicho, Hayati Dk. John Magufuli, kuingilia kati akiagiza kikokotoo hicho kipya kianze kutumika mwaka 2023.

Aprili 6, mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan, aliweka wazi kuwa PSSSF iko katika hali mbaya kifedha, akisema: "Ninajua hali ya PSSSF, kuwa mfuko huu una hali mbaya na ndiyo maana sikuteua mtu. Hapa tuna kazi ya kufanya kwanza kunusuru mfuko ule halafu ndiyo tujue sasa safu ipi ya kushika huo mfuko."

Mfuko huo ni zao la kuunganishwa kwa mifuko minne ambayo ni: PPF, PSPF, LAPF na GEPF.

Katika hotuba yake ya Jumanne, Majaliwa pia alisema serikali itaendelea kuisimamia Sekta ya Hifadhi ya Jamii kwa kuhakikisha Sera ya Kinga ya Jamii inakamilika.

Alisema ofisi yake itaendelea kutekeleza majukumu yote yaliyoainishwa katika Sheria ya Hifadhi ya Jamii, ili kuhakikisha taasisi zote za Hifadhi ya Jamii zinafuata kanuni na miongozo iliyopo ili kupunguza kero kwa wananchi wanaowahudumia.

# Spika asema uaminifu unazidi kupungua nchini

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amesema uaminifu miongoni mwa vijana unazidi kupungua nchini, akiitaka serikali kuchukua hatua kukabiliana na mmomonyoko wa maadili.

Alisema hayo bungeni jijini Dodoma jana wakati wa kuhitimisha mjadala wa mwelekeo wa serikali na makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka ujao wa fedha.

Spika Ndugai alisema ipo haja serikali kuchukua hatua kukabiliana na mmomonyoko huo wa maadili, akisisitiza kuwa vijana wengi sasa wamekosa uaminifu.

Alisema kuna haja viongozi wa dini pia walione suala hilo na kuangalia njia za kuwasaidia vijana, ili kuwa na taifa lenye maadili na uaminifu mkubwa.

"Ukitaka kulijua hilo, nenda tu kule mtaani mpe kijana mradi ausimamie, usipokwenda kuangalia kinachoendelea kwa miezi, ukija kwenda, ukikagua hesabu, umepigwa.

"Vijana hawajui kwamba ukiaminika kwenye kitu kidogo, utaaminika hata kwenye mambo makubwa.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu tulione hili," alisema.


NYADHI INVESTMENT Co. LIMITED

TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

M/MWANZO MJINI - SHAURI LA MADAI Na. 367/2020

AGNES RAPHAEL MGOSI.......................MDAI
DHIDI YA
SELESTINE ROBERT..........................MDAIWA

M/MWANZO MJINI - SHAURI LA MIRATHI Na. 89/2018

HALIMA GEORGE PASTORY...............MWOMBAJI DHIDI YA
GEORGE PASTORY.........................MAREHEMU

M/MWANZO MISUNGWI - SHAURI LA MADAI Na. 15/2019

PILI ATHUMAN MASAZA ..........................MDAI DHIDI YA
UNDI TANGA JILALA..........................MDAIWA

KWA IDHINI NA MAMLAKA TULIYOPEWA NA MAHAKAMA YA MWANZO MWANZA MJINI, MAHAKAMA YA MWANZO MISUNGWI, TUNAUZA KWA MNADA WA HADHARA MALI ZA WADAAWA AMBAZO NI NYUMBA. MNADA UTAFANYIKA MAHALA MALI ILIPO.

| SN | MALI INAYOUZWA | MAHALI | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | NYUMBA | NYUMBA ILIYOKO KIWANJA NA. 2877 KITALU "A" ILIYOKO NYASAKA CENTA | 18/5/2021 SAA 3 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 2 | NYUMBA | NYUMBA ILIYOKO MABATINI MWANZA | 18/5/2021 SAA 5 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 3 | NYUMBA | MTAA WA NYALUHAMA-BUHONGWA | 19/5/2021 SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |

MASHARTI YA MNADA:
1. MTEJA ATALIPA ASILIMIA ISHIRINI NA TANO YA BEI ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA NA ITAKAYOSALIA ATALIPA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE. KUSHINDWA KUFANYA HIVYO MTEJA ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI YAKE YA MSINGI NA MNADA UTARUDIWA TENA.
2. GHARAMA ZOTE ZITAKAZOJITOKEZA BAADA YA KUNUNUA MALI KWENYE MNADA NI JUU YA MNUNUZI.

MAWASILIANO: 0768-588155/0782-405140



TANGAZO LA MNADA

**WORK ETHIC INVESTMENT CO.** Kwa niaba ya MZALENDO CREDIT,- Tutauza kwa mnada wa hadahara Dhamana ya Mdaiwa sugu aliyetajwa hapo chini baada ya kushindwa kulipa deni kwa muda mrefu.

| NO. | JINA LA MDAIWA | DHAMANA/SIFA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| | MOSES KIBABU MFUNDO | KIWANJA NO.74, KITALU NO.6, HATI NO.142541 | JUMATATU TAREHE 03.05.2021 |

MASHARTI YA MNADA
A. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili kutoka.
B. Mnunuzi atakayeshinda atalipa 25% au zaidi ya bei ya mnada na salio la 75% litalipwa ndani ya siku 14.
C. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa muda uliotolewa,atakuwa amepoteza haki zote na kiwanja(dhamana) itauzwa tena

KWA MAELEZO ZAIDI WASILIAN NASI KWA SIMU NAMBA 0713 801904/0623662447/0787917366

HABARI KITAIFA

# Hoseah aibuka mshindi urais TLS

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA



ALIYEKUWA Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), Dk. Edward Hoseah (pichani), ameshinda kiti cha Urais wa Chama cha Wanasheria Tanzania (TLS), baada ya kumbwaga mpinzani wake kwa tofauti ya kura 40.

Dk. Hosea anatajwa kama mtu muhimu aliyekuwa akipewa nafasi kubwa dhidi ya wapinzani wake kurejesha heshima ya chama hicho, alipata kura 297, huku mpinzani wake, Wakili Flaviana Charles, ambaye ni Mkurugenzi wa Kituo cha Bussness & Human Rights Tanzania akipata kura 223 .

Akitangaza matokeo hayo jana jijini hapa, Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi, Wakili mkongwe nchini, Charles Rwechungura, alisema waliojiandikisha kupiga kura kumtafuta Rais mpya wa TLS kwa mwaka 2021/22, walikuwa 5,286 lakini waliopiga kura ni 802.

Idadi kubwa ya wanachama wa TLS wanaofikia 4,477 hawakupiga kura hiyo.

Wagombea wengine waliojitosa kuwania kiti hicho na kura walizopata kwenye mabano ni Wakili Shehzada Walli (192), Wakili Albert Msando aliyeambulia kura 69 wakati Rais wa zamani wa TLS, Wakili Francis Stollah, aliambulia kura 17.

Katika matokeo hayo, Wakili Gloria Mandes, sasa anakuwa Makamu wa Rais wa chama hicho baada ya kuchaguliwa kwa kura 324.

Alisema wamefurahi kwa niaba ya kamati kwa uchaguzi mzuri usio na vurugu na walioshinda wataapishwa kesho.

**OSEAH ANENA MAZITO**

Akizungumza mara baada ya kutangazwa kushinda nafasi hiyo Dk. Hosea aliwashukuru wapiga kura na kamati ya uchaguzi kwa kufanya uchaguzi mzuri wa huru na haki.

Alisema uchaguzi huo ulikua ukifuatiliwa nchi mzima, kwa sababu sekta ya sheria ni ya muhimu katika maisha ya watu.

"Kazi kubwa ya TLS ni kusimamia utawala wa sheria, mahakama zilizo huru hivyo nitashirikiana na wenzangu kuhakikisha misingi ya sheria inafuatwa kwa kushirikiana na bunge na mahakama,"alisema.

Alisema atapenda kuona kila mtu yupo huru katika macho ya sheria na isibague mtu kwa rangi wala cheo.

"Mahakama lazima ziwe huru na kufanya uamuzi huru na hata serikali pia na kazi hii naamini tutashirikiana ili mihimili hii ifanye kazi yake vyema,"alisema.

Alisema Watanzania wategemee TLS kufanya kazi zake kwa uwazi bila kujali umri au rangi ya mtu na anaamini serikali iliyopo madarakani ni sikivu na atafanya nayo kazi nzuri.

"Kuna jinsi ya kuzungumza na mkubwa au serikali nitatumia uzoefu wangu kuzungumza nao na mambo yataenda vizuri,"alisema

# Waziri Mkuu aanika mikakati uwekezaji

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, ametaja mikakati ambayo serikali imechukua kuhakikisha wawekezaji wanalindwa na vibali vyao vinafanyiwa kazi pasi na urasimu wala rushwa.

Vilevile, amewatoa hofu Watanzania kuhusu kuendelezwa kwa Makao Makuu ya nchi Dodoma kwa kuwa serikali imeweka mfumo mzuri utakaohakikisha miundombinu mbalimbali inajengwa kwa mujibu wa sheria ya mipango ya maendeleo ya Jiji la Dodoma.

Majaliwa alitoa kauli hiyo bungeni jana wakati akijibu hoja mbalimbali zilizotolewa na wabunge wakati wa mjadala wa mwelekeo wa kazi za serikali na makadirio ya hotuba ya ofisi yake na taasisi zilizo chini yake kwa mwaka ujao wa fedha.

Alisema katika masuala ya wawekezaji, watafanya mabadiliko ya sera na sheria zake ikiwamo kufanya mabadiliko ya masharti mbalimbali kuhusu vibali vya kazi kwa wawekezaji.

Waziri Mkuu alisema Rais ameielekeza ofisi hiyo kuimarisha huduma za pamoja, kushughulikia malalamiko yote kuhusu kodi, kuondoa vikwazo katika uwekezaji, kuhamasisha uwekezaji kupitia mazungumzo, kudhibiti rushwa na kuondoa urasimu kwenye maeneo yote ya uwekezaji.

Alisema baada ya kutolewa kwa maagizo hayo, tayari hatua mbalimbali zimechukuliwa zikiwamo kuandaa muundo wa wizara ambao utaainisha majukumu ya mgawanyo wa idara na taasisi zitakazokuwa chini ya eneo la uwekezaji.

Majaliwa alisema wanapitia upya Sera ya Uwekezaji ya Mwaka 1996 na Sheria ya Mwaka 1997, ili kubainisha maeneo yenye uhitaji wa maboresho ambapo tayari tathimini ya utekelezaji wa sera ya taifa imekamilika.

"Pia, tunaandaa mkakati wa kitaifa wa maendeleo ya uwekezaji ili kuimarisha utaratibu, usimamizi, uhamasishaji na ufuatiliaji wa masuala ya uwekezaji katika sekta zote nchini," alisema.

Majaliwa alisema kuwa kukamilika kwa hatua hizo kutaiwezesha serikali kutekeleza masuala muhimu kama kushiriki kikamilifu katika mikutano na majadiliano ya jumuiya na kikanda yanayohusu masuala ya uwekezaji yakiwamo maandalizi ya sera ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Alisema serikali itajenga mazingira rafiki ya wawekezaji na uchumi shindani nchini na kutekeleza programu mbalimbali za kuimarisha mazingira hayo.

Alisema kuwa katika kuhakikisha hali ya uwekezaji inaimarika, wameandaa mfumo wa kielektroniki wa kupokea na kushughulikia malalamiko ya wawekezaji pamoja na kutatua vikwazo vinavyowakabili wafanyabiashara kupitia Baraza la Taifa la Biashara ambalo linaundwa kuanzia ngazi ya wilaya, Mkoa na taifa ambalo mwenyekiti ni Rais.

Majaliwa aliagiza fursa za uwekezaji zilizopo kwenye maeneo mbalimbali, ziibuliwe na wananchi waelimshwe namna ya kupata wabia ili kushirikiana nao, pia kuimarisha mifuko ya kutoa cheti cha ushiriki wa miradi ya maendeleo.

Aliwakumbusha watendaji wakiwamo mawaziri, makatibu wakuu na manaibu wao kuhakikisha muundo na mifumo ya masuala ya uwekezaji unafanyiwa kazi ndani ya muda uliowekwa na Rais.

"Ninasisitiza kuwa watendaji wajiepushe na uombaji wa rushwa, urasimu usiotakiwa katika kuwahudumia wawekezaji ili kujenga imani baina ya serikali au sekta ya umma na sekta binafsi, ili tuweze kuzungumza lugha moja," aliagiza.

00000


## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **NSOMBO COMPANY LIMITED,MAK RECOVERIESLTD na MBUXAZ AUCTION MART** Kwa idhini tuliyopewa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD** tunatoa muda wa siku 14 kwa wadaiwa walioorodheshwa kwenye jedwali hapo chini wawe wamelipa madeni wanayodaiwa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD,** Kinyume na hapo tutalazimika kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara mali walizoweka kama dhamana ya mkopo. Tarehe za kufanya minada zitatolewa kwa njia ya vipeperushi na magari ya matangazo kwenye sehemu dhamana zilipo.

**NOTISI KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

| S/N | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA |
|---|---|---|---|
| | **MAK RECOVERIESLTD** | | |
| 1 | MHINA M MUHONDOMEO | GARI, MITSUBISHI ROSA NO T-616 DGZ, PLOT BLOCK N0 209 | PONGOWE TANGA |
| 2 | OMAR RAJABU OMAR | NISSAN CIVILIAN NA. T 690 DDR | TANGA CITY |
| 3 | JOSEPHAT MMASI | MITSUBISHI FUSO NAMBA T 746 BAE | TANGA CITY |
| 4 | RAPHAEL VENSESLAUS SHAYO | PIKIPIKI NAMBA MC 499 CEW | TANGA CITY |
| 5 | FRANCIS J SEMKIWA | TOYOTA LAND CRUISER NA. T 128 AZW | MABOKWENI TANGA CITY |
| 6 | YUSTA YOHANA MHANDO | KIWANJA | TANGA CITY |
| 7 | BAKARI M KISENA | TOYOTA CARINA NAMBA T 854 CES | MABOKWENI TANGA CITY |
| 8 | SHABANI M MBAGA | MITSUBISHI FUSO NAMBA T 666 AAW | MUHEZA TOWN |
| | **MBUXAZ AUCTION MART** | | |
| | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA |
| 9 | FATUMA HABIBU ABDALLAH | NYUMBA | PUGU CORNER - DAR ES SALAAM |
| 10 | ELISIA M. MUSHI | NYUMBA | KIMARA TEMBONI - DAR ES SALAAM |
| 11 | DOMINICK N MSILA | NYUMBA | BOMBAMBILI - DAR ES SALAAM |
| 12 | ABDALLAH M MISANGO | NYUMBA | VINGUNGUTI - DAR ES SALAAM |
| 13 | MCHENI SAIDI BAKARI | NYUMBA | MBAGALA CHARAMBE - DAR ES SALAAM |
| 14 | PETER N. NYAWAYA | NYUMBA | KITUNDA - DAR ES SALAAM |
| 15 | BAKARI RAMADHANI ALMAS | NYUMBA | MSONGOLA - DAR ES SALAAM |
| 16 | WILFRED LUCAS NYATO | NYUMBA | BOMBAMBILI - DAR ES SALAAM |
| | **NSOMBO COMPANY LIMITED** | | |
| 17 | HASSAN R MWENDAPOLE | TOYOTA NOAH REG: T266 BNL, FIXED ASSETS AND HOUSEHOLD | SHINYANGA |
| 18 | HANILAIDA S MWITA | PLOT NO. 29 BLOCK "PP" VIWANJA VYA MWADUI, Home Chattel and Fixed Assets | SHINYANGA |
| 19 | JOSEPH R MFOI | PLOT NO. 51 BLOCK "K" MAGANZO HOME CHATTEL | MAGANZO , SHINYANGA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
3. Mnunuzi atayeshinda anapaswa kulipa 25% ya bei aliyofikiwa siku ya mnada, na 75% iliyosalia atalipa ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada, Kinyume na hapo kiasi kilichotolewa awali hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha Hati miliki (Transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa ni la mnunuzi.
5. Mnada utafanyika mahali ambapo dhamana zilipo na si vinginevyo.

Mkurugenzi Mtendaji
Nsombo Company Limited
P.o.box 40632
Dar es Salaam
Na
Mkurugenzi Mtendaji,
Mack Recoveries Ltd
0715 375475/ 0783224965
0716 35 3650/0763 481 798

Na
Mkurungezi Mtendaji,
Mbuzax auction Mart Company limited
P.O.Box 62070
Na
Finca Microfinance Bank ltd
P.O.Box 78783
Mobile: 0768790399, 0754774949

# RC aombwa kuingilia kati mgogoro ardhi

**Na Gideon Mwakanosya,** NAMTUMBO

WANANCHI kutoka koo 16 katika Kijiji cha Mchomoro, Namtumbo mkoani Ruvuma wamemwomba Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christine Mdeme, kuingilia kati mgogoro wa ardhi wa zaidi ya ekari 700 kati yao na aliyekuwa Mkuu wa Wilaya hiyo, Luckness Amlima.

Kwa mujibu wa wananchi hao, kuendelea kwa mgogoro huo kumesababisha kuzorota kwa shughuli za kimaendeleo.

Wakizungumza na waandishi wa habari waliofika katika kijiji hicho juzi, wawakilishi wa koo hizo zenye takribani familia 70, walisema mgogoro huo umedumu kwa zaidi ya miaka minne sasa na kwamba viongozi wa kijiji na wilaya wamekuwa wakipuuzia kwa sababu zao binafsi, huku wakiwatuhumu kumpendelea kiongozi huyo mstaafu.

Mmoja wa wawakilishi wa koo hizo, Rashid Malamaye, alidai kuwa kiongozi huyo alivamia katika maeneo yao ya asili ambayo walikuwa wanayatumia kwa shughuli za kilimo na ufugaji kwa miaka mingi lakini cha kushangaza kwa sasa wanataka kudhulumiwa.

Malamaye alisema katika mashamba hayo kulikuwa na nyumba za nyasi lakini zimechomwa moto, mazao ya muda mrefu aina ya minazi, michungwa, migomba na mihogo na kwamba mazao hayo yamefyekwa bila wao kujulishwa na kuwekwa walinzi ambao wamekuwa wakiwapiga wananchi wanaokwenda katika mashamba hayo.

"Tumeshtushwa sana na kitendo hicho cha uharibifu wa mazao yetu na uvamizi wa mashamba ambayo yapo katika maeneo ya mahane katika kitongoji cha Nyerere na mwekezaji ambaye aliwahi kuwa mkuu wa wilaya bila sisi wenye maeneo kujulishwa. Hata tulipolalamika kwenye uongozi wa kijiji na wilaya, hakuna hatua zinazochukuliwa dhidi yake," alisema Malamaye

Naye Issa Languka alisema kuwa baada ya kutokea kwa uvamizi huo, walitoa taarifa katika uongozi wa kijiji na kwenye uongozi wa Chama Cha Mapinduzi(CCM) lakini majibu waliyoyatoa ni kwamba mwekezaji huyo yupo kihalali bila kufafanua sheria ipi au mkutano gani wa hadhara ambao ulihalalisha zaidi ya ekari 700.

Languka alisema inasikitisha kuona viongozi wa kijiji badala ya kulinda raia na mali zao, wamekuwa chanzo cha kutengeneza migogoro kinyume cha kiapo chao cha uadilifu. "Kutokana na kitendo hicho, tumemwandikia Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christine Mdeme, kumjulisha madai yetu ili achukue hatua kwani mwenendo wa viongozi wa wilaya kuhusu mgogoro huu hauridhishi na hatuna imani nao," alisema.

# Wafanyabiashara wadaiwa kero kwa abiria stendi mpya Mbezi

**Na Maulid Mmbaga**

ONGEZEKO la wafanyabiashara katika Kituo cha Mabasi cha Magufuli kilichopo eneo la Mbezi Luis mkoani Dar es Salaam, kumetajwa kuwa ni kero kwa wasafiri wanaofika katika kituo hicho.

Februari 24, mwaka huu Hayati Rais John Magufuli wakati akizindua kituo hicho, alitoa ruhusa kwa wafanyabiashara wadogo kufanya shughuli zao ndani ya kituo hicho.

Lakini kuruhusiwa kwa wafanyabiashara hao, kumesababisha usumbufu kwa wasafiri, kwamba wanafanya biashara hadi katika maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya wasafiri kupumzika.

Wakizungumza na Nipashe, mmoja wa abiria, Iddy Mushi, alisema kitendo cha wafanyabiashara kujazana katika stendi hiyo kinashusha hadhi ya kituo hicho ambacho katika matengenezo yake kiliigharimu serikali zaidi ya Sh. bilioni 50.

Alisema katika baraza zilizotengwa kwa ajili ya abiria kusimama wakati wakisubiria usafiri, kwa sasa panaonekana kama soko kutokana na msongamano mkubwa wa wafanyabiashara uliopo.

"Ukitazama hili eneo lilivyo sasa hata ile heshima ya stendi imepungua, hivyo tunaomba serikali ilitazame hili kwa ukaribu iweke utaratibu utakaosaidia kuondoa tatizo hili biashara ifanyike lakini kwa utaratibu maalum," alisema.

Moja wa mawakala wa mabasi, Hashimu Ally, aliiambia Nipashe kwamba kuna baadhi ya abiria wanalazimika kusubiri usafiri ndani ya magari kutokana na baadhi ya wafanyabiashara kuvamia ghorofa ya pili ambayo ipo maalumu kwa ajili ya wasafiri kupumzika, zilipo ofisi za mawakala wa mabasi.

"Abiria wanapata taabu na wengine wanaona shida hata kufika katika eneo hili hivyo tunauomba uongozi kuangalia njia nyingine mbadala ya kuwapanga hawa wafanyabiashara kwa usahihi kwani wakati mwingine inatuwia ngumu kumtambua abiria," alisema Ally.

Mkurungenzi wa Manispaa ya Ubungo, Beatrice Dominic, alisema Aprili 19, mwaka huu wafanyabiashara wadogo pamoja na wauza chakula watahamishwa na kupelekwa katika jengo ambalo liko nyuma ya kituo hicho ambalo ujenzi wake unamalizika.

Alisema utaratibu wa kuwahamisha ukikamilika, kutawekwa utaratibu maalumu wa kuhakikisha ni mfanyabiashara gani atakayeruhusiwa kuingia kufanya biashara katika stendi hiyo.

Alisema baadhi ya wafanyabiashara hao watahamishwa ili kutoa nafasi kwa wamiliki wa mabasi kutumia ofisi zilizopo ndani ya kituo kukatia tiketi na waachane na ofisi za nje.




Mkazi wa Nzega, Habiba Bushiri, akifurahi baada ya kukabidhiwa pikipiki ya magurudumu matatu na Benki ya NMB, kwa kuibuka mshindi wa promosheni ya Bonge la Mpango, wakati wa hafla ya makabidhiano iliyofanyika mkoani Tabora juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAMWA yazindua kampeni ya kuzuia ukatili mitandoni

**Na Beatrice Shayo**

CHAMA Cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), kimezindua kampeni ya 'Zuia Ukatili Mtandaoni' ambayo inalenga kupinga vitendo vya ukatili na udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto wa kike mitandaoni.

Kadhalika, kimetoa wito kwa serikali na asasi za kiraia kuzungumzia madhara ya vitendo vya ukatili wa mitandao na kutoa elimu kwa jamii ili kuondoa tatizo hilo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Dar es Salaam, Sylvia Daulinge, kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa TAMWA, Rose Reuben, alisema ukatili wa mtandao umekuwa ukiwaathiri zaidi watoto wa kike na wanawake kutokana na namna ya makuzi na desturi za jamii.

Daulinge alisema takwimu za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) zinaonyesha kuwa kuna ongezeko kubwa la watumiaji wa mtandao mpaka mwaka 2017 watumiaji waliongezeka kwa asilimia 16 na kufikia idadi ya milioni 23.

"Tumeona mara kadhaa video za utupu za wanawake, watoto wakike zikisambazwa katika mitandao hiyo. Tumeshuhudia matukio ya video za ngono za wanawake zikisambazwa kwa makusudi kabisa, huu ni udhalilishaji unaofanyika kwa njia ya mtandao,"alisema.

Daulinge alisema udhalilishaji huo una madhara kisaikolojia na kusababisha watu kuathirika kisaikolojia na wengine kujiua au kupoteza mwelekeo katika maisha.

"Bado udhalilishaji huu unaendelea pengine ni waathirika kutoifahamu sheria hii au kuona aibu katika kutafuta haki au hofu ya kudhalilika zaidi kesi itakapopelekwa mahakamani," alisema.

Alisema TAMWA haikubali udhalilishaji huo, ni muhimu wananchi wakatambua sheria zinawalinda, kwamba kuna adhabu kwa wanaotumia mitandao ya kijamii vibaya ikiwamo faini ya Sh. milioni tano au kifungo kisichopungua miezi 12 au kwa vyote kwa pamoja.

Mrakibu Mwandamizi wa Polisi, Dawati la Jinsia na Watoto Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Leah Mbunda, alisema kampeni hiyo itasaidia kuleta chachu katika jamii katika kuwoangezea wananchi uelewa.

Alisema wapo ambao wanadhalilishwa katika mitandao ya kijamii wanakaa kimya na wengine kuona aibu.

HABARI KITAIFA

# Uwekezaji bil. 35/- kupunguza uhaba wa saruji

**Na Joseph Mwendapole**

KIWANDA cha saruji cha Twiga kinatarajia kuwekeza Dola za Marekani milioni 15 sawa na Sh. bilioni 35 kwa ajili ya kukarabati mitambo na kukiongezea uwezo wa uzalishaji.

Hayo yalisemwa jana na Meneja Biashara Mwandamizi wa Kampuni hiyo, Danford Semwenda, wakati ujumbe wa Kituo cha Uwekezaji Tazania (TIC) ulipotembelea kiwanda hicho kilichoko Wazo, Dar es Salaam.

Ujumbe huo ulitembelea kiwanda hicho kwa ajili ya kujionea shughuli za uzalishaji na kusikia changamoto mbalimbali ambazo wawekezaji hao wanakabiliana nazo ili wazitatue.

Semwenda alisema wamekuwa na changamoto ya kucheleweshewa shehena ya mizigo yao bandarini hali ambayo husababisha mizigo yao kukaa muda mrefu na kutozwa faini kubwa.

"Uwekezaji unaofanyika hapa ni mkubwa sana hivyo tunahitaji watu kama TIC waje wasikilize kero zetu na kwa kweli tumefurajia ujio wao hapa kwasababu umeonyesha namna gani walivyotayari kutusaidia," alisema Semwenda.

Aidha, alisema kiwanda hicho kimekuwa kikilipa kodi serikalini zinazofikia Sh. bilioni 54 na kutoa ajira kwa maelfu ya vijana wa kitanzania. Pia alisema kwenye awamu ya tano, kiwanda hicho kilifanya biashara kubwa ya saruji.

Semwenda alisema miradi ya kimkakati iliyotekelezwa kwenye awamu ya tano ilisababisha saruji kuhitajika kwa wingi hali iliyosababisha wapate faida na kuongeza gawio kwa wanahisa wake kwa asilimia 40.

Bevin Ngenzi, Meneja wa TIC Kanda ya Mashariki, alisema wameamua kutembelea kiwanda hicho kujua kinavyoendelea na uzalishaji na kuangalia changomoto waanazokalian nzo ili waweze kuzitatua.

Alisema TIC imefurahi kusikia kuwa kiwanda hicho kimekuwa kikiongeza uwezo wake wa kuzalisha kila mwaka hali ambayo imesidia serikali kupata kodi kubwa na watanzania wengi kupata ajira.

Ngenzi alisema miaka 10 iliyopita kiwanda hicho kilikuwa kikizalisha tani milioni 1.2 kwa mwaka na sasa uwezo wake umeongezeka hadi kufikia tani milioni mbili kwa mwaka.

"Wawekezaji hawa wanaendelea vizuri na wameishukuru serikali kwa mazingira mazuri ila kuna changamoto ndogo ndogo za kisera ambazo tunakwenda kuzifanyia kazi haraka," alisema Ngenzi.

Alisema mwekezaji huyo ameelezea changamoto ya kuchelewesha mizigo bandarini hivyo watakwenda kukaa na taasisi husika kuhakikisha changamoto hiyo inafanyiwa kazi.

Alisema kazi ya TIC ni kuhakikisha wawekezaji wanafanya biashara katika mazingira mazuri na tulivu hivyo wataendelea kutembelea viwanda na kampuni ili kusikiliza kero mbalimbali.




Katibu Msaidizi kutoka Umoja wa Waendeshaji wa vituo vya mafuta nchini (TAPSOA) Maulid Mahfudh, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati wakitangaza kuungana na kampuni ya Tigo, ambapo wateja wataweza kufanya malipo ya mafuta kwa Tigo Pesa kupitia lipa namba 777512. Kulia ni Ofisa Mkuu wa Huduma za Kifedha wa Tigo, Angelica Pesha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ashanti, Umoja zaingia ubia uchimbaji madini

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Anglogold Ashanti imeanzisha ubia na BG Umoja na kuipatia mkataba wenye thamani ya dola za Marekani milioni 186 kwa miaka miwili katika miradi ya uchimbaji ya Nyankanga na Geita Hill.

Lengo la ubia huo limetajwa kuwa ni kuzingatia mpango wa kuongeza mchango endelevu katika uchumi wa jamii inayozunguka mgodi.

Ubia huo wa asilimia 80 kwa 20 ni ushirikiano kati ya kampuni ya Africa Underground Mining Services (AUMS) ya Tanzania, kampuni tanzu ya kundi la Perenti Australia na kampuni ya huduma za uchorongaji wa ndani na usambazaji madini ya Geofields Tanzania Limited.

Ushirikiano huo utafanyika sawa na muundo wa ushirikiano uliotekelezwa katika uchimbaji wa chini kwa chini katika Mgodi wa Obuasi nchini Ghana kati ya AUMS Ghana na kampuni iliyoko Accra - inayomilikiwa na Waghana ya Rocksure, ushirikiano utakaojenga uwezo wa uchimbaji maalumu ndani ya nchi.

Akizungumzia ubia huo, Ofisa Uendeshaji Mkuu wa AngloGold Ashanti Afrika, Sicelo Ntuli, alisem: "Tunafanya kazi na makandarasi wa uchimbaji wenye uzoefu watakaotusaidia kuwezesha uhamisho wa muda mrefu wa ujuzi endelevu, na kuendelea kujenga mipango endelevu ya ununuzi wa ndani.

"AngloGold Ashanti inajenga mipango endelevu ya ununuzi wa ndani utakaochochea maendeleo ya uchumi na jamii katika miradi, inayoshuhudiwa na mchango mkubwa kutoka Geita Gold Mining Limited ambao umechangia mapato makubwa ya watu wa Tanzania."

Alisema matumizi ya mwaka ya AngloGold Ashanti kwa watoa huduma Watanzania wazawa yameongezeka hadi dola milioni 162 kuanzia mwaka 2016.

"Timu ya kusimamia ununuzi wa ndani imejiwekea malengo makubwa ya asilimia 60 hadi 70 ya matumizi yote kufanywa na kampuni za Kitanzania nchi ifikapo 2025."

" Kampuni ya AngloGold Ashanti - Geita Gold Mining Limited imetoa pia mkataba wa miaka miwili wa usafirishaji mafuta wenye thamani ya dola milioni 10.8 kwa mwaka kwa kampuni mbili za Kitanzania. Mojawapo ya kampuni kati ya mbili zitakazonufaika katika mkataba huo ina asili ya Geita na inathibitisha ahadi ya GGML kuwezesha uchumi wa jamii wenyeji," alisema.

Alisema kampuni ya Geita itakayonufaika katika mpango huo imepatikana baada ya jitihada za GGML kushirikiana na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) kutoa mafunzo wezeshi kwa watoa huduma wa Geita ili kuongeza wigo wa kushindana katika ununuzi na utoaji huduma unaofanywa na Mgodi.

" Katika kufikia viwango ya kimataifa, malori ya kubeba mafuta hayo yamepewa mwongozo wa kuzingatia utoaji moshi kwa mujibu wa viwango vya EURO IV, matangi yanapaswa kutengenezwa kwa kutumia aluminium ili kupunguza uzito na kila gari litapaswa kutumika katika kipindi kisichozidi miaka sita.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Usajili wachezaji wapya msimu ujao uanze sasa

**WASWAHILI** wanasema kila lenye mwanzo halikosi kuwa na mwisho. Kwa sasa Ligi Kuu Tanzania Bara ndio inaelekea ukingoni zikiwa zimebakia raundi chache ili msimu wa mwaka 2020/21 umalizike.

Dalili za kumalizika kwa msimu huu zimeshaonekana tayari kwa timu kugawanyika katika makundi matatu.

Kundi la kwanza ni lile ambalo kuna timu zinazowania ubingwa wakati kundi la pili ni lile la timu ambazo ziko katika nafasi salama ambazo zenyewe haziko kwenye vita ya kuwania ufalme na zimeshaondoka katika hatari ya kushuka daraja.

Kundi la tatu ni la timu zilizoko katika mstari mwekundu wa kushuka daraja au kucheza mechi za mtoano ambazo pia huzungukwa na presha kutoka kila upande.

Hata hivyo katika soka lolote linaweza kutokea na hivyo Nipashe inazikumbusha timu zote 18 zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi Daraja la Kwanza, Ligi Daraja la Pili na Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania kutokata tamaa na badala yake kupambana kusaka matokeo chanya mpaka katika mechi ya mwisho ya funga pazia.

Mbali na timu zinazoshiriki ligi hizo kwa upande wa Tanzania Bara, pia timu zote zinazoshiriki ligi mbalimbali zinazosimamiwa na Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), zinatakiwa kuendelea kujituma kwa kuongeza umakini na utulivu katika dakika hizi za lala salama ambazo zinaweza kubadilisha msimamo uliopo sasa na kuwaweka nafasi nzuri.

Wachezaji na makocha huu ndio wakati wenu wa kujiweka sokoni kwa kujituma na kuonyesha viwango vya juu, kwa sababu kwa kufanya hivyo kutawaongezea thamani kuelekea msimu ujao wa 2021/22.

Kwa maana hiyo, Nipashe inazikumbusha timu zote kutumia udhaifu na upungufu ulioonekana katika msimu huu kwa ajili ya kujiimarisha kuelekea msimu mpya ili kutorudia makosa yale yale.

Ni wazi timu itakayofanya maandalizi yake vizuri na mapema, itajiweka katika mazingira ya kuwa imara na yenye kutoa ushindani katika msimu mpya, lakini pia wachezaji na wamiliki wasiangalie maslahi ya upande mmoja.

Huu ni wakati wa kila timu na kila mchezaji kuwa na 'kiu' au 'wivu' wa maendeleo kwa kujipanga kusaka timu mpya au kujiongezea thamani kwa klabu unayoitumikia sasa kwa kupewa mkataba mpya mnono kama uliopo umemalizika au kuruhusu mazungumzo ambayo utapelekea kupandishwa mshahara.

Umefika wakati timu zikabadilisha mwonekano kwa kujiimarisha na kuonyesha ushindani na kuacha kusindikiza wenzao kwa muda mrefu tangu zilipopanda daraja na kushiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya kwanza.


Katika kipindi hiki ambacho zimebakia raundi nane kumalizika kwa msimu huu, tunaamini makocha watakuwa tayari wameshabaini nafasi ambazo wanahitaji kuziboresha kwenye vikosi vyao na hatimaye msimu ujao kuingia wakiwa washindani

Ukiondoa vita za timu kwa timu, huu ni muda mwafaka wa wamiliki wa klabu kujipanga kuboresha mabenchi ya ufundi na hatimaye kumaliza unyonge wa kupoteza idadi kubwa ya mechi katika msimu mpya na kumaliza 'ubabe' wa muda mrefu unaofanya na timu au zinazojiita kongwe kwenye ligi hiyo.

Kupata sifa ya kushiriki Ligi Kuu, basi ujue pia unaweza kuiwakilisha nchi katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika au Kombe la Shirikisho, hivyo kufanya maandalizi ya kusajili kikosi imara mapema, ndio dalili za kufanya vyema katika msimu ujao.

Mafanikio katika soka au mchezo wowote kamwe hayapatikani kwa njia ya miujiza, timu au wanamichezo walioandaliwa kwa kufuata misingi bora, ndio wenye nafasi ya kunyakua mataji au kupata matokeo bora na si vinginevyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wadau, wawekezaji katika soka wasikatishwe tamaa

Na Adam Fungamwango

**HIVI** karibuni, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, pamoja na mambo mengine alitaka wawekezaji kuwekewa mazingira mazuri nchini ili kuwavutia waweze kumiminika kwa ajili kupata mafanikio.

Rais huyo alisema kuwa wawekezaji wasibughuziwe, badala yake wawekewe utaratibu unaoeleweka ili wajue kama wanataka kuwekeza wanalazimika wafuate taratibu zipi na si kuwazungusha na mambo mengine yanayofanana na hayo.

Siku chache baadaye, Mbunge wa Makete (CCM), Festo Sanga naye akiwa bungeni alitaka wawekezaji kwenye mpira wa miguu nchini walindwe na kutoruhusu watu kuwashambulia.

Lakini baada ya siku chache tena, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Klabu ya Simba, Mohamed Dewji 'Mo' aliandika kwenye mtandao wake wa kijamii kutoridhishwa na mchakato wa mabadiliko ya uendeshaji wa klabu hiyo jinsi unavyoendeshwa na Tume ya Ushindani ya Biashara (FCC).

Pamoja na mambo mengi, Mo alikuwa na wasiwasi kuwa huenda ikawa kuna baadhi ya watu wana mpango wa kuchelewesha mabadiliko hayo kutoka mfumo wa kizamani wa kutegemea wanachama na kuendeshwa kama kampuni.

Mo aliandika kuwa wanakutana na kufanya vikao, lakini walipokaribia waliambiwa waanze tena.

Mfumo wa mabadiliko ya Simba ulianza tangu mwaka 2017 kwa wanachama wenyewe katika Mkutano Mkuu kuridhia kubadilisha katiba ya klabu yao kwa kupiga kura na kujiendesha kisasa.

Awali, wanachama walitaka kumpa Mo asilimia 51, lakini serikali ilipinga na kutaka wawekezaji kuchukua asilimia 49 na kiasi kilichobakia kiwe kwa wanachama.

Serikali ilikubali mfumo wa uendeshaji kwa sababu iliona ule mfumo wa kutegemea wanachama hauwezi kuziendesha klabu vizuri kulingana na ushindani uliopo.

Zamani, Serikali ilibeba mzigo huo kwani wachezaji wengi hasa wa timu za Simba na Yanga walikuwa waajiriwa na kampuni na mashirika ya umma, huku kwenye soka wakicheza kama ridhaa tu, walipata posho za mazoezi, mechi na safari.

Lakini soka kwa sasa dunia nzima limebadilika, mpira sasa ni kazi rasmi, hivyo wachezaji wanalipwa mamilioni ya soka kama mshahara, na klabu za wanachama haziwezi kumudu gharama hizo.

Simba imekuwa timu ya kwanza kutaka kubadilika ili zingine zifuate, lakini FCC imeonekana kama kuchelewesha mchakato huo.

Inawezekana Simba ikawa na makosa kwenye mchakato huo, lakini kinachotakiwa ni FCC kuwaambia kinaga ubaga nini cha kufanya na nini hakitakiwi kifanyike badala ya kuonekana kama kuna kuviziana au mwingine kuonekana anamkwamisha mwingine. FCC kama mmoja ya Taasisi za Serikali inapashwa kuisaidia Simba kwa kuweka wazi nini wanapaswa kufanya, ili mchakato huo imalizike kwa manufaa ya soka la Tanzania kwa ujumla.

Ni kwa sababu klabu nyingi sasa zinaitazama Simba kama klabu ya mfano na ikishafanikiwa na wao wataanza, hivyo kuchelewa kunafanya nazo zisite kufanya hivyo.

Lakini pia ikumbukwe kuwa wawekezaji kwenye soka ni wachache sana na wanahitajika zaidi kwenye soka la Tanzania, hivyo hawa wachache waliokuwapo kama Mo wangetengenezewa mazingira rafiki ili wengine waone soka ni sehemu sahihi ya kwenda kuwekeza.

Kuonekana kama wanazungushwa au hawatakiwi, kunaweza kufanya wakakimbia na soka likaendelea kudidimia.

Kwa sasa Simba inafanya vyema kwenye mechi za kimataifa, huku ikiwa kwenye mchakato huo, je kama ikifanikiwa si unaweza kuwa faida kwa taifa siku moja Rais Samia ikabidhiwe Kombe la Ubingwa wa Afrika?

Mimi nadhani tutengeneze kanuni za kuwawezesha wawekezaji kukimbilia na kujiingiza kwenye soka na si kanuni za kutaka washindwe na kukimbia, tutakuwa hatuutendei haki mpira wa Tanzania na taifa kwa ujumla kwani ikikwama Simba basi timu nyingine hazitoweza kuthubutu kufanya mabadiliko.

Tusidanganyane, kwa sasa mabadiliko timu kwenda kwenye uendeshaji wa kisasa ni suala la lazima, kwani kwa sasa soka linahitaji pesa nyingi, dunia nzima imebadilika na Tanzania siyo kijiji. Hakuna soka la ridhaa kwa sasa ambalo litaendeshwa na wanachama kwa pesa za michango na malipo ya kadi za uanachama. Kwa sababu kwa sasa hakuna mchezaji anayefanya kazi Shirika la Bima halafu anachezea Simba au Yanga kama ilivyokuwa zamani.



Mbunge Viti Maalum, Mkoa wa Geita, Rose Busiga, akichangia bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, bungeni jijini Dodoma jana.
**PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wabunge wapanda bodaboda watahadharishwa

BAADHI ya wabunge wanaotumia usafiri wa bodaboda kwenda bungeni na kurudi nyumbani, wametahadhariwa kuwa makini na madereva wanaowaendesha kwa kuwa kupatikana kwao ni kwa gharama kubwa.

Spika wa Bunge, Job Ndugai, alitoa angalizo hilo jana wakati wa kipindi cha maswali na majibu kwenye swali linalohusu ujenzi wa barabara.

Akizungumza baada ya Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya, kujibu swali la Mbunge wa Kibaha Vijijini (CCM), Michael Mwakamo, Ndugai alitumia nafasi hiyo kuwaasa wanaotumia usafiri huo kuwa makini kwa kuwa anazo taarifa baadhi ya wanakuja bungeni kwa usafiri huo.

"Ule usafiri ni mzuri kabisa kwa wananchi. Sina shida nao lakini basi nawaomba umakini na kuwa na uhakika wa huyo dereva anayeendesha maana kupatikana kwenu ni kwa gharama kubwa. Nadhani mmenisoma, nashukuru sana na pia ni vizuri kuelewa kuwa wananchi wakikuona huko watatafsiri vipi," alisema.

Awali, akatika swali lake, Mbunge Mwakamo, alihoji lini serikali itaanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Makofia hadi Vikumburu wilayani Kisarawe.

Katika majibu yake, Kasekenya alibainisha barabara hiyo yenye urefu wa kilometa 135.97 ni ya mkoa inayounganisha wilaya za Bagamoyo, Kibaha na Kisarawe. "Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina pamoja na uhakiki wa mali zitakazoathiriwa na mradi wa sehemu ya Makofia - Mlandizi - Maneromango yenye urefu wa kilometa 100 umekamilika," alisema.

Alibainisha kuwa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hiyo utaanza baada ya kupata fedha ambazo serikali inaendelea kutafuta.

"Wizara yangu inaendelea kuihudumia barabara hiyo ili kupitika majira yote ya mwaka. Katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya Sh. milioni 1,524.07 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo mbalimbali,"alisema.

# Sababu kuchelewa uendelezaji maliasili ukanda kusini zatajwa

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, ametaja sababu za kuchelewa kukamilika kwa mradi wa kuendeleza maliasili na kukuza utalii Kusini mwa Tanzania (REGROW) kuwa ni kutokana na vikwazo mbalimbali ikiwamo kuchelewa kuanza kwa majadiliano ya utekelezaji kwa takribani miezi 17.

Masanja aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Ritta Kabati, ambaye alihoji utekelezaji wa mradi huo utaanza lini.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri alisema pamoja na kikwazo hicho, pia uwapo wa COVID - 19 umechangia kwa kiasi kikubwa kuendelea kuchelewesha utekelezaji kutokana na kazi nyingi kusimama.

"Ili kukabiliana na changamoto zilizojitokeza, mradi umefanyiwa mapitio ya kati ambapo miongoni mwa mambo mengine ni kuongeza muda wa utekelezaji wa mradi hadi mwaka 2025 ili kufidia muda uliopotea," alisema.

Alifafanua kuwa mradi huo tayari ulianza kutekelezwa tangu mwaka 2017 na unatekelezwa kwa mkopo wa Dola za Kimarekani milioni 150 kutoka Benki ya Dunia.

"Maeneo ya kipaumbele ni hifadhi nne za taifa (Ruaha, Mikumi, Nyerere na Udzungwa) na maeneo yanayozunguka hifadhi hizo pamoja na eneo la chanzo cha maji cha Mto Ruaha Mkuu," alisema.

Alisema mradi huo unatekelezwa kwa kipindi cha miaka sita kuanzia mwaka 2017 hadi 2023 na hadi kufikia mwezi Machi 2021, mradi huu umeendelea kutekelezwa kwa ufanisi mkubwa.

"Kazi zifuatazo zimetekelezwa ununuzi wa vifaa vya doria, magari 44 na mitambo mikubwa mitatu kati ya 18. Pia mradi umeajiri kampuni sita ambazo zinaendelea na usanifu wa majengo, barabara na viwanja vya ndege,"alisema.

# Sera, sheria uvuvi kufanyiwa mapitio

BUNGE limeelezwa kuwa serikali iko tayari kupitia upya sera na sheria ya uvuvi nchini ili kukidhi mahitaji yaliyopo kwa wavuvi wadogo.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alibainisha hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Neema Lugangira.

Katika swali lake, Mbunge huyo alitaka kujua kama serikali iko tayari kupitia sera na sheria hiyo ambayo inaonekana kutokidhi mahitaji ya wavuvi wadogo.

Akijibu swali hilo, Ulega alisema serikali iko tayari kupitia sera na sheria ya uvuvi na katika kulitekeleza hilo, wizara imekuwa ikifanya mapitio ya sera, sheria na kanuni za uvuvi ili kuendana na mahitaji halisi ya wakati husika na imekuwa ikifanya hivyo mara kwa mara.

Ulega alitolea mfano wa wizara kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Uvuvi na mikakati yake ya mwaka 1997 na kutunga Sera ya Taifa ya Uvuvi ya mwaka 2015 ambayo imezingatia mahitaji ya wadau wa sekta ya uvuvi na uendelevu wa rasilimali za uvuvi.

Alisema wizara ilifanya mapitio ya Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania Na. 6 ya Mwaka 1980 na kutunga Sheria Na. 11 ya Mwaka 2016 ili kuimarisha shughuli za utafiti nchini.

"Mwaka 2020 Wizara ilifanya marekebisho madogo (Miscellaneous ammenments) kwenye Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 ili kuimarisha shughuli za ulinzi na usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi nchini," alisema.

Aliongeza kuwa wizara inaendelea kufanya maboresho makubwa kwenye Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 ili kuendana na mahitaji halisi ya sasa ya kisekta ikiwemo kutatua kero mbalimbali za wadau wa uvuvi, hususan wavuvi wadogo na wakuzaji viumbe maji.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA

# RC aipongeza BRELA kutoa elimu kwa umma

**Na Mwandishi Wetu,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, ameipongeza Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) kwa kufika katika mkoa huo kutoa elimu kwa umma.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua semina ya siku mbili ya elimu kuhusu huduma zinazotolewa na taasisi hiyo kwa wakazi wa Singida.

Katika hotuba ya ufunguzi wa semina hiyo, Dk. Nchimbi alisema amefurahishwa na ujio wa BRELA mkoani humo kwa kuwa hiyo italeta hamasa kubwa kwa wajasiriamali na wafanyabiashara kurasimisha biashara zao kwa kuzisajili.

"Kuna elimu nyingi zinazotolewa, lakini elimu ya BRELA inathamani kubwa sana kwa maendeleo ya taifa letu. Niliposikia mnakuja mkoani Singida nilifurahi sana kwa kuwa badala ya wananchi kuwafuata ninyi ndio mmewafuata wananchi," alisema Nchimbi.

Dk. Nchimbi alisema Singida ya sasa si kama ile ya zamani, kuna fursa nyingi za uwekezaji na idadi ya wafanyabiashara na wajasiriamali imekuwa ikiongezeka siku hadi siku.

"Singida kwa miaka mingi imekuwa ikionekana si mkoa wa kibiashara, lakini leo nimefarijika sana kuona kwamba mmefika katika mkoa huu, hii inamaanisha mmeona kwamba wapo wafanyabiashara na Wajasiriamali wa kutosha" alisema.

Naye Ofisa Leseni Mwandamizi kutoka BRELA, Abbas Cothema, alisema kwa mwaka 2020/21 taasisi iliweka mikakati kadhaa moja wapo ikiwa ni kutoa elimu kwa umma kuhusu majukumu yake, huduma inazotoa (kabla ya usajili na baada ya usajili), namna ya kuzipata huduma hizo kwa njia ya mtandao katika mikoa mbalimbali.

Alisema kwa awamu ya kwanza mikoa ambayo itafikiwa ni pamoja na Singida na Ruvuma, Dodoma na Njombe na kumalizia , Morogoro na Iringa.

# Shirika latia saini mkataba bil. 5.6/

**Na Frank Monyo**

SHIRIKA la Legal Services Facility (LSF), limetia saini mkataba wa kupokea ruzuku ya Sh. bilioni 5.6 kutoka Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Denmark (DANIDA), kwa ajili ya kutekeleza mradi wa upatikanaji wa haki kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Ruzuku hiyo ni nyongeza kwa ajili ya kutekeleza mradi wa upatikanaji wa haki unaolenga kuboresha mazingira ya uwezeshaji wa kisheria nchini, kwa kuzijengea uwezo taasisi zinazotoa huduma ya msaada wa kisheria, huduma za wasaidizi wa kisheria nchini kwa makundi mbalimbali katika jamii hususani wanawake na watoto.

Akizungumza wakati wa hafla ya kutilia saini jijini Dar es Salaam, Balozi wa Denmark nchini Tanzania, Mette Norgaard Dissing-Spandet, alisema kuwa DANIDA imeamua kuwaongezea ruzuku LSF kwa kipindi cha mwaka mmoja ikiwa ni sehemu ya uwajibikaji katika kuhakikisha suala la upatikanaji wa haki nchini Tanzania linazingatiwa.

"Tunaamini ruzuku hii itasaidia katika kuboresha mifumo ya utoaji haki iliyo rasmi na isiyo rasmi ili kuwezesha upatikanaji wa haki kwa wakati, lakini pia kuwezesha upatikaji wa sera na sheria bora zinazolinda maslahi ya Watanzania hususani wanawake na watoto," alisema balozi huyo na kuongeza;

"Ufadhili huu ni sehemu yetu katika kuhakikisha kuwa jamii yote nchini Tanzania inakuwa na utawala wa sheria unaoheshimu kila mtu bila kujali umri au jinsia".

Alisema mradi huo unalenga kujenga msingi endelevu wa huduma za msaada wa kisheria nchini kwa kupitia upya mifumo, sera, na sheria kandamizi zinazorudisha nyuma ustawi na maendeleo ya wanawake na watoto katika jamii.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa LSF, Lulu Ng'wanakilala, alisema ruzuku iliyotolewa na wadau hao itasaidia katika kuendelea kutekeleza mradi wa upatikanaji wa haki nchini.

"Ikumbukwe kwamba miezi sita iliyopita DANIDA walitoa ruzuku kwa LSF Sh. milioni 71 ili kuwezesha elimu ya mpiga kura na usimamizi wa uchanguzi kwa mashirika 31 yaliyopewa vibali na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuendesha shughuli hizo za uchaguzi," alisema Ng'wanakilala.

Alisema katika kipindi cha miaka mitano iliyopita LSF imekuwa ikishirikiana na wadau ikiwamo DANIDA, ambayo imesaidia kuboresha sekta ya msaada wa kisheria nchini kupitia uwezeshaji wa kisheria kwa kuyapa ruzuku mashirika zaidi ya 200 yanayotoa huduma za msaada wa kisheria.



Mkuu wa Mkoa wa Singida, Rehema Nchimbi (katikati), akizungumza wakati akifungua semina ya utoaji wa elimu kwa umma, iliyoandaliwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), mkoni humo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mfanyabiashara kortini madai ya kujeruhi mteja

**Na Samson Chacha, TARIME**

MFANYABIASHARA wa duka la kuuza pombe katika mji mdogo wa Sirari., mkoani mara, Marwa Wainenga, amefikishwa katika Mahakama ya Wilaya Tarime akishtakiwa kutaka kumuua mteja wake, Simon Machugu kwa kumpiga risasi.

Inadaiwa kuwa alimuua Simon aliyekuwa akinywa Pombe na wenzake kwa kumpiga Risasi na kumjeruhi vibaya Pajani na kumsababishia maumivu makali Akisomewa mashtaka mbele ya Hakimu Mkazi Veronica Mugendi, Mwendesha Mashitaka wa Polisi, Bugombe Bukulu, alidaiwa alimpiga risasi Machungu akiwa anakunywa pombe na wenzake, na kumjeruhi vibaya pajani na kumsababishia maumivu makali.

"Mtuhumiwa alifanya tukio hilo la kumshambulia na kumpiga risasi pajani mteja wake, Machugu usiku wa Julai 7, 2020 wakati Machugu alipokuwa akinywa vinywaji katika 'grocey' ya mtuhumiwa baada ya kutokea mzozo kati yake na wateja.

"Hatua hiyo ilisababisha Wainega kutoa bastola na kumpiga risasi pajani majeruhi Machungu na kupelekwa Hospitali ya Wilaya Tarime na kulazwa," alidai mwendesha mashtaka.

Mtuhumiwa Wainenga alikana mashitaka hayo na kupewa dhamana.

Upande wa mashitaka ulidai upelelezi unaendelea na kesi hiyo itatajwa tena Mei 13, mwaka huu.

Mwendesha mashtaka Bukulu alidai kuwa silaha inayodaiwa kutumia katika tukio hilo, inashikiliwa na Jeshi la Polisi.



# TMX kutojihusisha minada mazao

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Kilimo, imesema katika msimu mwa kilimo mwaka huu, Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) halitajihusisha na shughuli za minada ya mazao.

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alitoa kauli hiyo jana bungeni baada ya wabunge kulalamikia TMX kuvuruga minada ya mazao na kuitaka iendelee na majukumu yake na si kujihusisha na minada.

Bashe alisema: “Tunafanya tathmini ya ujumla wasiwe na hofu majaribio yaliyofanyika mwaka jana tumeona athari. Tumefikia uamuzi ushirika utaendelea kufanya shughuli zake za ushirika na TMX itarudi kufanya kazi zake.”

Awali, wakichangia hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2021/22, Mbunge wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota, alisema katika minada iliyofanywa kupitia TMX hadi sasa, baadhi ya wakulima hawajalipwa fedha zao.

“Wakulima wa korosho na ufuta hutumia akaunti zao za benki wakati wa msimu na baada ya miezi sita haipo hai na matokeo yake fedha zikipelekwa benki zinakuta akaunti ipo dormant (haifanyi kazi).

Kwa hiyo kwa mfumo wa stakabadhi ghalani, mkulima anakimbilia kwa kiongozi wake wa chama cha ushirika inakuwa rahisi kutatua tatizo na kupata fedha zake, lakini kwa TMX hadi leo wakulima wanadai fedha na bado hawajapata,” alisema na kusisitiza mfumo huo unaonekana wazi kuwa na kero.

Naye Mbunge wa Itilima (CCM), Njalu Silanga, alisema serikali ina nia ya dhati katika kutengeneza ushirika, AMCOS na TMX lakini TMX imekuwa ikifanya kazi ya kwenda kijijini kusimamia ushirika na kuchukua asilimia moja ya bei inayopatikana jambo hili haliwezekani linawaumiza wakulima.

Alisema TMX inatakiwa kutafuta masoko nje ya nchi na si kazi hii inayofanywa na taasisi hiyo.

“Miaka ya nyuma kulikuwa na chombo kinaitwa Mamlaka ya Pamba ambacho kilipewa jukumu la kuuza pamba zote nchini lakini yaliyotokea shirika lile lilikufa na kuleta madhara makubwa na hatima yetu leo shirika lilifilisika kwa sababu ya vyombo hivi TMX wameanza tangu mwaka 2018 na mwaka 2019 tukaingia katika tatizo la kukosa masoko ya pamba,” alisema.

“TMX nilidhani ingeonyesha njia kubwa kuhakikisha kwamba wanauwezo wa kutafuta masoko na kuuza mazao yao lakini matokeo yake hakuna kilichofanyika na serikali iliingilia kati kutatua changamoto hiyo.

“Naibu Spika ningeomba sana serikali ijaribu kuangalia inapoleta mipango mizuri hasa inayoenda kwa wananchi wetu tuelewe asilimia 70 ya Watanzania ni wakulima na wafugaji,” alisema.



Ofisa Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna (kushoto), akizungumza na wafanyabiashara wa soko jipya la Makole, jijini humo jana, wakati akiwatoa hofu ya kuondolewa kwenye eneo hilo. Wengine ni Diwani wa Kata ya Makole, Omary Omary (wa pili kushoto) na (wa tatu kushoto) ni Mwenyekiti wa Mtaa wa Makole, Anni Ngaya. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# RC ataka ushirikishaji afya lishe

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, ametaka viongozi wa vijiji na mitaa kushirikishwa kwenye masuala la lishe na afya ya mzazi ili kupata mwitikio mzuri kwa jamii.

Dk. Mahenge alisema hayo jana jijini hapa katika kikao cha mapitio ya viashiria vya huduma za afya ya uzazi na mtoto, pamoja na tathmini ya nusu mwaka ya utekelezaji wa viashiria vya mkataba wa lishe.

Alisema viongozi wa vijiji na mitaa ni watu muhimu kwa kuwa ndio wanaowajua watu vizuri.

“Hili suala ni muhimu sana ili lifanikiwe lazima tuwashirikishe wadau, na wadau wenyewe ni viongozi wa vijiji na mitaa hawa watatusaidia ndio wanaishi na hawa watu, wao ndio wanajua nyumba gani kuna mjamzito,” alisema.

Alisema pamoja na juhudi zilizofanywa na Serikali ya Mkoa kuanza kuleta matumaini bado hawajafikia lengo lililotakiwa la kumaliza kabisa tatizo la lishe duni na huduma ya afya ya uzazi.

“Kwa kweli tumejitahidi kwa kiasi fulani lakini hatujafikia lengo. Lengo ni kuona katika ripoti hatuna alama za njano au nyekundu na hili linawezekana kila mmoja kwenye eneo lake akitimiza wajibu wake,” alisema.

Aliwasisitiza Wakurugenzi wa Halmashauri zote kuhakikisha wanatenga fedha kama walivyoagizwa ili kupunguza utapiamlo.

Awali, akiwasilisha ripoti kwenye kikao hicho, Mratibu wa Huduma za Afya ya Uzazi wa Mtoto Mkoa wa Dodoma, Nice Mosha, alisema wamekuwa wakitoa mafunzo mbalimbali kwa watumishi katika kutekeleza elimu ya uzazi wa mpango.

“Wataalamu wanatuambia kuwa watoto waliopata huduma bora kilishe kipindi cha siku 1,000 za mwanzo wa uhai wao wanapata faida zitakazodumu katika maisha yao yote na pamoja na maendeleo mazuri ya ukuaji wa ubongo na uwezo mzuri wa kukabiliana na maradhi,” alisema.

Kuhusu tawimu za vifo vya uzazi na mtoto, alisema kwa mwaka 2018 ilikuwa 67, mwaka 2019 ilikuwa 74, na mwaka 2020 ikawa 88 huku takwimu za vifo kwa watoto wachanga mwaka 2019 ilikuwa 694, na 2020 ikawa 681 ambapo ilishuka kidogo.

Ofisa Lishe wa Mkoa wa Dodoma, Herieth Carin, alisema Oktoba 18, 2018 walitia saini mkataba wa afua za lishe na wamekuwa wakitekeleza kupitia halmashauri na wao wametia saini mikataba hiyo hadi ngazi za chini kuhakikisha wanatimiza malengo ya afua za lishe kuondoa tatizo la lishe katika jamii.

Alisema halmashauri zimekuwa zikitenga fedha ili kutekeleza masuala mbalimbali ya lishe na kila halmashauri zimekuwa zikitakiwa kutenga Sh. 1,000 kwa kila mtoto katika masuala ya lishe.

## Ufafanuzi

KATIKA toleo letu la Aprili 9 mwaka huu, tulichapisha habari yenye kichwa kinachosomeka ‘Lukuvi aombwa kibali cha ujenzi Chang’ombe’, ikiwanukuu wananchi na viongozi wa Mtaa wa Mtakuja Mjimwema jijini Dodoma wakimwomba Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, kuruhusu ujenzi wa nyumba kwenye maeneo hayo.

Julai 15, mwaka jana, Lukuvi aliagiza kusimamishwa kwa ujenzi wa nyumba kwenye eneo hilo kwa madai kuwa kampuni iliyolipima ya J.F ilikuwa haitambuliwi kisheria na serikali na imeshafutwa.

Hata hivyo, ufuatiliaji wetu umebaini mwandishi wetu aliunukuu vibaya uongozi wa serikali za mitaa kwenye eneo hilo kuhusu suala hilo.

Pia, mkutano uliofanyika siku ambayo mwandishi aliwanukuu wananchi wakimwomba waziri huyo kuruhusu kibali, haukuwa maalum kwa ajili ya masuala ya ardhi, bali ulikuwa mkutano wa kawaida kwa mujibu wa taratibu za serikali za mitaa.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mtakuja, Hemed Seleman, ajenda za mkutano huo wa hadhara zilijumuisha kufungua mkutano, utambulisho, mapato na matumizi, lishe kwa kinamama wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka mitano.

Ajenga zingine zilikuwa ni ulinzi na usalama, taarifa mbalimbali zilizogusa umeme, ukarabati wa barabara kilomita kwa kiwango cha changarawe na kuwakumbusha wananchi kuhusu agizo la Waziri Lukuvi.

Mambo matatu yaliyoagizwa na Waziri Lukuvi ni pamoja na wananchi wahakikiwe katika maeneo yao, Seleman alibainisha kuwa uhakiki huo ulishafanyika.

Agizo la pili la Waziri Lukuvi ni wananchi kutouza maeneo yao wala kujenga mpaka atakaporejea kutoa majibu ya mwisho na la tatu ni kufutwa kwa hati zote zilizotolewa katika eneo hilo.

Nipashe tunauomba radhi uongozi wa serikali za mitaa katika eneo hilo na wasomaji wetu kutokana na usumbufu uliojitokeza.

**Mhariri**



# Serikali yaonya wanao kwamisha mawakala ajira

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

OFISI ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji imesema haitavumilia taasisi yoyote itakayokwenda kinyume cha taratibu zilizowekwa kisheria katika shughuli za wakala binafsi za ajira .

Hayo yalisemwa juzi na Kamishna wa Kazi, Fatma Iddi Ali, wakati akifungua mkutano wa kuzijengea uwezo taasisi binafsi za ajira kwenye ukumbi wa ofisi hiyo, Mwanakwerekwe kwa niaba ya Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji.

Fatma aliwataka mawakala binafsi kuzingatia sheria zilizopo zinazohusu shughuli zao bila kuziendea kinyume ili kuepuka changamoto zinazojitokeza.

Alisema wakala binafsi wa ajira wamepewa ruhusa kisheria kuwaunganisha waajiri na watafuta kazi kote duniani, hivyo katika kuendesha shughuli hizo, wahakikishe wanakuwa na taarifa za waajiri na watafuta kazi ili kusaidia kuondokana na matatizo mbalimbali.

Aliwasisitiza mawakala hao kupeleka wananchi wenye elimu ya kujitambua, ujuzi na uwezo wa kazi badala ya kuchukua yoyote pamoja na kufuatilia taarifa za watu waliosafirishwa na kutoa taarifa haraka linapotokea tatizo.

"Msifanye kazi kwa tamaa, jalini kuwa hii ni kazi rasmi inayotambuliwa na serikali. Hakikisheni mnakidhi masharti na maelekezo ya sheria na kanuni pamoja na kushirikiana na balozi zetu za Tanzania nje ya nchi," alisema.

Alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inafahamu umuhimu wa taasisi hizo za wakala binafsi wa ajira na inathamini juhudi zao kwani inasaidia kwa kiwango kikubwa kupunguza tatizo la ajira kwa vijana.

Naye Kaimu Mkurugenzi Idara ya Ajira ambae pia ni Mkurugenzi Idara ya Usalama Kazini, Suleiman Khamis Ali, alisema ajira 8, 1161 zimepatikana nje ya nchi tangu utaratibu wa wakala wa ajira kuanza mwaka 2012.

Alisema hadi sasa kuna taasisi za wakala binafsi wa ajira zipatazo 15 ambazo zinatambulika kisheria.

Nao mawakala hao waliiomba Idara ya Ajira na Kamisheni ya Kazi kuzungumza na waajiri binafsi wakiwamo wawekezaji kwa kuwa inaonekana hawajafahamu dhana ya kuwapo mawakala wa ajira ili kushirikiana na kufikia lengo lililokusudiwa na serikali.



Mhasibu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, Seif Ahmed Kombo, akimtilisha saini ya kidole, Namboto Ali Haji, wakati wa ulipaji fidia ya maeneo yao yaliyochukuliwa na serikali kwa ajili ya kupisha ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kigunda, Mkoa wa Kaskazini Unguja jana. Wa (pili kushoto) ni Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini A, Sadifa Juma Khamis. **PICHA: HAWA ABDALLAH**

# Walipwa fidia kupisha ujenzi uwanja wa ndege

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

ZAIDI ya Sh. milioni 130 zimetumika kulipa fidia kwa wananchi waliochukuliwa maeneo yao ya kilimo kupisha mradi wa ujenzi wa uwanja wa ndege wa Kigunda Wilaya ya Kaskazini A, Kaskazini Unguja.

Akizungumza katika hafla maalumu ya ulipaji toaji fidia kwa wananchi hao iliyofanyika Gamba katika ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini A, Meneja wa Uwanja wa Ndege wa Kigunda, Fatma Mohammed Yussuf, alisema watu 281 watalipwa fidia hiyo.

Fatma alisema utoaji fidia kwa wananchi hao emeshafanyika kwa awamu sita hadi sasa na kuwatoa hofu wananchi wa maeneo hayo kuwa serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA) itahakikisha kila anayepaswa kulipwa stahiki hizo anapatiwa.

"Nitumie fursa hii kuwatoa hofu wananchi waliotoa maeneo yao ili kupisha ujenzi wa uwanja wa ndege kuwa kila anayestahili kupata haki hiyo, atapatiwa licha ya changamoto ndogo ndogo zilizojitokeza likiwamo suala la kufanyiwa uhakiki," alisema.

Fatma aliwaomba wananchi hao kuendelea kutoa ushirikiano kwa ZAA katika uendelezaji wa mradi huo kwa kuwa utaleta tija kubwa kwa taifa katika kukuza uchumi.

" Niwaombe sana wananchi zinapotokea fursa kama hizi za ujenzi wa miradi mikubwa ya serikali, watoe ushirikiano wa kutosha kwani miradi hii itakwenda kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi kwa mtu mmoja mmoja lakini pia kwa taifa," alisema.

Nao wananchi waliopata stahiki hizo walipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia ZAA kwa kuwapatia fidia hizo ambazo zitawasaidia kujiendesha kimaisha kwa kuimarisha maeneo mengine ya kilimo.

"Kwa kweli tunaishukuru serikali yetu kwa kutupatia fedha hizi kwa ajili ya malipo ya maeneo yaliyotumika kwa ujenzi wa uwanja wa ndege wa Kigunda maana yalichelewa kidogo na wengine tulihisi hatutolipwa. Maeneo yenyewe ni ya serikali lakini tunashukuru sana kwa kutujali sisi wanyonge kwa sababu maisha yetu tulio wengi tunategemea kilimo," walisema wananchi hao.

Akizungumza katika gafla hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini A, Sadifa Juma Khamis, alisema amefarijika kuona wananchi wake wamepokea stahiki zao ambazo walikuwa wakidai na kuwataka kuhakikisha harudi katika maeneo hayo badala yake watumie fedha hizo kuwekeza maeneo mengine.

"Kufanyika kwa ulipaji fidia kwangu ni faraja kubwa kwani nimekuwa nikipokea malalamiko kutoka kwa wananchi mara nyingi kuhusu malipo yao na mimi nilijaribu kufuatilia na kuwakumbusha viongozi wa mamlaka husika na walinipa matumaini ya kupatiwa stahiki hizi," alisema Sadifa.

# Waziri, wajumbe bodi watakiwa kujiuzulu

**Na Mwandishi Wetu**, PEMBA

VIONGOZI wa Bodi ya Udhibiti wa Vileo Zanzibar na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idaras maalum za SMZ baada ya sheria ya vileo namba 9 kuvunjwa na bodi hiyo.

Wito huo ulitolewa juzi na viongozi wa dini na wananchi katika kisomo cha dua cha kuombea amani Zanzibar na kulaani vitendo vya uvunjifu wa sheria kilichofanyika katika msikiti wa Ijumaa wa Uwandani na kuongozwa na Sheikh Ali Said Ali.

Kisomo hicho kilihudhuriwa na wananchi na viongozi wa dini kutoka vijiji na viongozi vya Uwandani, Mjanaza na Vikunguni wakiwamo na wanafunzi wa wa Madrasa Jimbo la Ole, Mkoa wa Kusini Pemba.

Akizungumza katika hafla hiyo, Ostadhi Kombo Ali Abdallla alisema wakati umefika Bodi ya Vileo kuvunjwa kutokana na kuvunja sheria ya vileo ya Zanzibar.

Sheikhe Kombo alisema wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar walipitisha sheria hiyo na kuanza kutumika baada ya kutiwa saini na Rais Mei 11, 2020 kwa madhumuni ya kudhibiti vileo lakini bodi imeshindwa kusimamia sheria hiyo.

"Kifungu cha 33(1) kinasema kibali cha kuagiza kitatolewa kwa waingizaji wasiozidi watatu kwa kuzingatia vigezo mwagizaji awe ni Mzanzibari, awe mlipa kodi lakini mpaka Febuari 22, kampuni nane zimepewa vibali vya kuingiza pombe Zanzibar," alisema.

Kombo alisema wameamua kufanya kisomo kulaani watendaji wote walioshiriki kuvunja sheria ya vileo bila kuchukuliwa hatua za kisheria na waziri mwenye dhamana. "Tunaomba serikali waivunje bodi yote ya kudhibiti vileo pamoja na viongozi kuwajibika kwa kushindwa kusimamia sheria, "alisema Kombo.

Pia alisema kifungu cha 28 (k) kimeweka masharti ya kutoa leseni kwamba lazima baa iwe umbali wa mita 1000 kutoka sehemu ya huduma za jamii kama shule, hospitali, nyumba ya ibada na madrasa lakini leseni zimeendelea kutolewa bila kujali masharti ya sheria hiyo.

Hata hivyo, alimpongeza Rais wa Zanzibar, Dk Hussen Ali Mwinyi, kwa kuendelea kuimarisha amani na mshikamano tangu kushika wadhifa huo.

Alisema Serikali ya Umoja wa Kitaifa imedumisha amani na kujenga misingi ya umoja wa kitaifa kwa wananchi wa Zanzibar tangu kumalizika kwa uchaguzi mkuu. Naye Ostadhi Khamis Rashid Hamad alisema wameamua kuitosha kisomo cha dua baada ya kushtushwa na kitendo cha bodi ya vileo kuvunja sheria bila viongozi waliopewa dhamana kuwachukulia hatua watendaji waliohusika akiwamo Mwenyekiti wa Bodi ya Vileo, Abdulrazak Abdulkadir.



**KANYE WEST** Uk.14
**AKUBALI YAISHE**

JUMAMOSI APRILI 17, 2021

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



**HAPA HAWATOKI**

# Harmonize kawaweka pabaya

ROHO zinawadunda wale walioshabikia na kujiingiza katika sakata la mwanamuziki wa Bongo Fleva, Harmanize na mkewe Kajala, kiasi ambacho wanatamani miujiza ili wasikabiliwe na mkono wa sheria.

Wahusika wengi wanatajwa kujiingiza katika sakata hilo ambalo limevuruga hali ya utulivu katika tasnia ya muziki nchini, na kusababisha Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA) kuingilia kati.

Harmonize amesema atasimama kidete kwa kuhakikisha watu waliomdhalilisha katika mitandao ya kijamii kwa kuweka video fupi inayomchafua, wanashikishwa adabu.

Amesisitiza hataki hata senti yao moja kama njia ya kumnyamazisha, bali wale wote waliohusika katika kutengeneza video inayosambaa mitandaoni wakidai kuwa muhusika ni yeye kwa lengo la kumchafua wanafikishwa mbele ya sheria.

Hivi karibuni katika mtandao wa Instagram kulikuwa na sintofahamu juu ya msanii huyo akihusishwa na tuhuma za kumtaka kimapenzi na mtoto wa mwenza wake Kajala Masanja ajulikanaye kwa jina la Paula. Inadaiwa alimtumia picha za mjongeo zilizo kinyume na maadili.

Harmonize alikanusha kuwa hakuhusika katika video hiyo inayosambaa mitandaoni na waliounganisha suala hilo walikuwa na lengo la kumchafua.

Rayvanny ambaye anahusishwa kwa kiasi kikubwa katika sakata hilo, hataweza kukwepa kwani akaunti yake ya Instagram amekuwa akitumia kuposti mambo mbalimbali kuhusu ugomvi huo.

Kwa upande wa mwanasheria wa Harmonize, Jorome Msekwa, kitendo ambacho mteja wake amefanyiwa ni makosa kisheria hivyo wanaandaa mashitaka ya kuwapeleka mahakamani wale wote waliohusika na suala hilo na watadai fidia ya mabilioni ya fedha.

"Tunawaonya wale wote wanaoendelea na ukiukwaji huu wa sheria dhidi ya mteja wetu na tunawataka waache kufanya hivyo mara moja na kabisa," amesisitiza.

BASI SAWA

## Wakazi aongoza kumtetea Gigy Money

RAPA mahiri nchini, Wakazi amejiunga katika kampeni inayolenga kuomba serikali kumfugulia mwanamuziki, Gigy Money, awe huru kufanya kazi.

Kampeni huyo inayofahamika kama 'Free Gigy Money' inashinikiza Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) kumwondolea adhabu ya kifungo cha miezi sita kutoshughulisha na sanaa.

"Kuna wasanii tena wakubwa wanafanya mambo ya ajabu, kinyume na maadili tuliyoyazoea, wanaachwa huru halafu Gigy Money ambaye alitumia ubunifu wa mavazi akashutumiwa yupo kinyume na maadili na kufungiwa miezi 6, Gigy Money ni mama na anategemewa na mtoto," amesema.



## Bilnass hataki kumgombanisha



MSANII wa muziki wa Bongo Fleva, Billnass amewataka mashabiki wake waache kuweka hisia zao katika wimbo wake mpya, huku akikanusha hajamuimba mtu.

Akizungumzia hilo kwenye kipindi cha Planet Bongo ya East Africa Radio, Billnass amesema wimbo wake utachukua muda kueleweka kwa sababu ni kazi inayoendelea.

"Ukiisikiliza hii stori na watu ambavyo wanaioanisha ni vitu viwili tofauti, inaweza ikawa inaoana lakini kuna utofauti sana, ni stori endelevu nitaidadavua vizuri kwa sababu ni stori inayoendelea," ameongeza.



## Rose umesema ya moyoni

MSANII mkongwe wa filamu, Rose Ndauka amesema kashfa nyingi zinazowaandama waigizaji imesababisha mashabiki wengi kuwatupa mkono.

Rose wakati walipoanza kazi ya uigizaji wakati huo hakukuwa na mitandao ya kijamii kama Instagram, WhatsApp wala Facebook, ila wasanii waliandamwa na kashfa au visa vingi.

"BongoMovie tumependwa sana na mashabiki na ujio wetu ulikuwa mkubwa sana, wakati tunatoka kulikuwa hakuna Instagram, Facebook wala WhatsApp ilikuwa ni rahisi kufanya vitu hata vikiwa vidogo ila vinachukuliwa kwa ukubwa kwenye jamii ila haimaanishi kwamba BongoFleva au tasnia zingine hazifanyi visa" ameeleza Rose Ndauka.



## Profesa Jay hanaga nongwa

MWANAMUZIKI mkongwe wa Bongo Fleva, Prof Jay, amekanusha kupigwa na msanii mwenzake Chidi Benz, akisema kingetokea kitendo hicho sawa na mbu kutoboa neti.

Prof Jay amesema alisukumizwa tu mbele ya watu wake hali ambayo kama angesema arudishe basi Chidi Benzi angetoboka kama neti.

"Chidi Benz ni mdogo wangu kabisa, nimemtengeneza na alikuwanyuma ya jukwaa upande wangu, aliletwa kwangu na Black Rhyno ila watu walimlisha madini hivyo akanyea kambi, hakunipiga ila alinisukuma kwenye mazingira magumu sana," amesema.

## Mwendo wa kusutana

**Na Adam Fungamwango**

Ni wiki ya pili sasa na inaenda ya tatu, kwenye mitandao ya kijamii hasa hapa nchini gumzo imekuwa ni mkasa wa msanii maarufu wa muziki wa kizazi kipya, bongo fleva, Harmonize, Kajala Masanja na binti yake Paula.

Awali, picha za mitandao wa kijamii zilikuwa zikiwaonyesha kama ni wapenzi wapya. Mmoja akasema ni wapenzi wa kupika na kupakua. Wakitembea na kusafiri huku na huko.

Kwa bahati mbaya sana penzi hilo likaingia kwenye rekodi ya kuwa moja kati ya penzi la mastaa lililodumu kwa muda mfupi zaidi. Inasemakana kwa sasa wametemana na kila mmoja akimshutumu mwenzake. Wapo wanaodai eti sababu jamaa alitaka kula kuku na mayai yake.

Sakata hilo linalozurura kwenye mitandao ya kijamii limesababisha kuibuke na ngoma tano mpya ambazo zote zinazungumzia jambo hilo. Hapa nia si kulidadavua sakata lenyewe, bali ni kuonyesha kuwa mtafaruku wa penzi hilo la Harmonize na Kajala limesababisha kuibuke na ngoma tano mpya ambazo ndizo tunaziangalia leo.

**Vibaya-Harmonize**

Mhusika mkuu mwenyewe, Haromize, Aprili 12, mwaka huu akatoa ngoma aliyoiita 'Vibaya'. Katika ngoma yake hiyo anamtahadharisha mpenzi wake juu ya walimwengu ambao wana tabia ya kusema mabaya ya wenzao ili wao waonekane wema. Anamwambia hata maadui zangu walikuwa maadui zako zamani.

Katika wimbo huo anasema hata ukisambaza picha zangu za aibu hujengi ila unaboMoa. Harmonize anaimba kuwa alikubali kuacha vya dezo kwa sababu ya penzi, akaachana na mzungu.

**Nyamaza-Rayvanny**

Kesho yake tu, Aprili 13, msanii Rayvanny alitoa ngoma iitwayo 'Nyamaza' ambayo inaonekana ni ya kumjibu Harmonize kwa kile alichokisema kwenye ngoma ya 'Vibaya'.

Rayvanny, ni mmoja kati ya walio katikati ya mzozo huo. Ni mmoja wa wahusika, anayehusishwa na Paula, binti wa Kajala.

**Harmo-Baba Levo**

Siku hiyo hiyo msanii mwingine Baba Levo naye akatoa ngoma yake aliyoupa jina la 'Harmo'.

Huyu yeye anaonekana kumshutumu mtu ambaye anaonekana alikuwa anamnyemelea msichana Paula. Kwa vyovyote vile yupo kwenye upande wa kina Kajala ambaye tayari wameshatemana na Harmonize.

**Hayakusuhu-Ibraah**

Katika kile kinachoonekana kuwa sakata hili si tu kwamba limewagusa wambeya wa kwenye mitandao ya kijamii, bali hata wasanii, kwani baada ya Baba Levo yeye kuwa upande wa kundi la kina Kajala, msanii Ibraah ambaye yupo kwenye kundi ya Konde Gang siku hiyo hiyo na yeye atatoa ngoma. Yeye katika wimbo huo unaonekana kabisa kuwa anamjibu Baba Levo kuwa 'Hayamhusu', kama lilivyo jina la ngoma yenyewe. Anamwambia aache kushindana na mwanajeshi. Anaweza akatimuliwa alipo na akasainiwa Gonde Gang, hivyo asiingilie mambo yasiyomhusu.

**Bifu la Nini-Besto Naso**

Msanii Besto Naso yeye Aprili 14 akaja na ngoma yake akaiita 'Bifu la Nini?' Huyu yeye amesimama kati. Hana upande kama wengine. Kwanza anaonekana kushangaa kila kona stori za Kajala, mara Paula na wamesahau kwamba wengine wako kwenye mfungo, kazi yao ni kurushiana madongo na kushangaa wasanii wanakwenda wapi sasa wakati wao wanatakuwa kuwa kioo cha jamii?

"Kuna mwingine katongoza mtoto kala mara penzi likanoga, wakajisahau kidogo, picha zikavuja, mtoto anamiliki ba'mdogo." Ni moja kati ya maneno yaliyo kwenye ngoma hiyo.



## Mission Town; Ukizingua, tunazinguana

**Na Adam Fungamwango**

HII filamu inaitwa 'Mission Town'. Ina mambo mengi ya kuangalia na kujifunza. Tutaangalia jinsi madawa ya kulevya wanavyokuwa janga kubwa kwenye dunia ya sasa. Tunaona jinsi baadhi ya askari polisi walivyopewa dhamana ya kulinda raia na mali zao, pamoja na kuzua uhalifu, wanapokuwa moja ya hao wahalifu.

Lakini pia jinsi mtu anavyoweza kufanya lolote lile, hata kwa kukiuka taaluma yake kwa ajili ya kuilinda familia yake. Tunajifunza jinsi baadhi ya watu tunaowaamini, lakini wao ndiyo wanaweza kukuangamiza. Pia tutaona jinsi watu wema wenye nia nzuri na jamii na taifa letu kwa ujumla wanapogeuka wao kuwa kama wahalifu na hatari ya kupoteza maisha inakuwa juu yao.

Imechezwa na wasanii Kassim Mkoka, Almasi Said, Grace Mapunda, Lucky Lukamo, Omari Lyombe, Emari Daudi na wengineo.

Mr. Matty ni mkuu wa genge na kuingiza na kusambaza madawa ya kulevya nchini ambaye ana mtandao hadi kwa baadhi ya maaskari na maofisa polisi, hivyo hakamatiki.

Askari mmoja anadhulumiwa mgawo wake na kuamua kutoa siri kwa mwandishi wa habari Feruzi. Mwandishi huyo anaamua kulianika genge hilo kwenye gazeti. Hapo ndipo tafrani inapoanza.

Mr. Matty analituma genge lake kumtafuta mwandishi huyo. Wanachofanya ni kumteka mke wa mhariri wa gazeti. Mhariri Marko anapigiwa simu ofisini kuambiwa mkewe ametekwa na wanachotaka ni jina la mwandishi wa habari aliyeandika habari hiyo. Pamoja na kwamba hatakiwi kufanya hiyo, lakini aliwapa ili mkewe aachiwe.

Faruzi anakamatwa, lakini bado watekaji waliendelea kumshikilia Maria mke wa mhariri.

Kama vile haitoshi, wanamteka pia mhariri, pamoja na mpenzi wa mwandishi Feruzi.

Kitu ambacho walikuwa hawakijui ni kwamba mpenzi wa mwandishi, Tunda ana uwezo mkubwa kwenye sanaa ya mapigano. Anafanikiwa kutoka. Anakwenda nyumbani kwa mhariri na kukutana na kijana wake Emari ambaye pia baba na mama yake wametekwa. Emari pia ni mzuri kwenye sanaa za mapigano.

Wanaamua kuungana na kuanza kulisambaratisha kundi lote la Mr.Matty kwa ajili ya kuwaokoa wapendwa wao. Emari baba na mama yake, Tunda mpenzi wake Feruzi.





# Kanye West akubali yaishe

RAPA bilionea Wa Marekani, Kanye West hatimaye amekubali ombi la kumpatia talaka mke wake Kim Kardashian.

Kulingana na mtandao wa TMZ, mwanamuziki huyo ameitaka mahakama kumpatia ruhusa ya kisheria kuwatunza watoto wake wanne.

Hata hivyo, bado matunzo ya watoto hao haitakuwa sawa, kutokana na wakati mwingi wataishi na mama yao.

Fununu kwamba wanandoa hao hawako vizuri zilianza kujitokeza Januari mwaka huu, na haikuchukua muda Kim aliwasilisha maombi ya talaka mahakamani.





## Bruno Iwuoha hatunaye tena

MWIGIZAJI mkongwe kutoka Nollywood, Bruno Iwuoha, amefariki dunia akiwa na umri wa miaka 68.

Kwa mujibu taarifa kutoka kwa Mkurugenzi wa Mawasiano na Uigizaji wa Nigeria, Monalisa Chinda Coker, amesema Bruno alifariki Aprili 10 mwaka huu.


"Ni uzuni kutaarifu kifo cha mkongwe wa sanaa ya uigizaji Bruno Obinna Iwuoha,alifariki asubuhi kutokana na matatizo ya kisukari" amesema Monalisa.

## Mrembo wa AKA afa ghorofani

MCHUMBA wa mwanamuziki wa Afrika Kusini, AKA anayefahamika kwa jina la Nelli Tembe, amefariki dunia baada ya kuanguka kutoka ghorofani.

Tukio hilo limetokea Aprili 11, mwaka huu, ambapo Nelli alianguka kutoka ghorofa ya 10 ya hotel ya Pepperclub iliyopo katikati ya jiji la Cape Town.

Polisi wa jimbo la Western Cape, Kepteni Frederick van Wyk, amesema tukio hili linahusishwa na uhalifu kutokana na mazingira ya kifo chake.







## JLO, Rodriguez mpo 'siriazi' kweli?

MWANAMUZIKI wa Marekani, Jennifer Lopez maarufu kama 'J Lo,' amevunja rasmi uchumba na Alex Rodriguez.

Katika taarifa yao ya pamoja iliyotolewa juzi, wenzi hao wa zamani wamesema kila mmoja atakuwa atafuata njia tofauti lakini watabaki kuwa marafiki.


"Tumegundua kuwa sisi ni marafiki, tutaendelea kufanya kazi pamoja na kusaidiana kwenye biashara na miradi yetu ya pamoja," walisema katika taarifa yao.

## The Game huo ndo uwanamume

RAPA mkali wa Marekani, The Game, ametoa somo kwa wanandoa akisema si jukumu la mwanamke kulipa gharama za ndani.

Amsema hata kama mwanamke ana uwezo wa kifedha, bado wanahitaji kutunzwa na kupewa pesa za matumizi.

The Game, amesema kwa upande wake hatamruhusu mwanamke wake kujihudumia wakati yeye yupo.



MAKALA

# NGOZI NYEUSI DAWA

## •Inahimili magonjwa kuliko nyeupe

Na Christina Mwakangale



NGOZI ni kiungo muhimu mwilini ambacho kazi yake ni kufunika viungo vya mwili.

Pia ni kati ya milango mitano ya fahamu ya mwili wa binadamu ambayo hufanya kazi tofauti ikiwamo kutoa ulinzi.

Ipo dhana kwa baadhi ya watu kwamba rangi nyeusi ya mwili haina mvuto, haivutii na baadhi huamua kupaka mafuta kuibadili iwe nyeupe.

Ngozi ina umuhimu na zipo sababu ambazo huathiri utendaji kazi wa mwili, ikiwamo joto, baridi, na wakati mwingine hutokea maradhi.

Bingwa wa Magonjwa ya Ngozi na Zinaa, Dk. Elias Kenene wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), anasema kuna aina takribani sita za ngozi.

Anasema mojawapo ni watu weupe (wazungu), mweupe wa kati, maji ya kunde, mweusi wa kati, mweusi wa wastani na mweusi sana (waafrika).

Dk. Kenene, anasema kadri ngozi inavyokuwa nyeusi ndivyo kiwango cha ulinzi na kupambana na athari tofauti ikiwamo mionzi ya jua ama joto huwa kikubwa.

"Madhara ya kupata katika ngozi inategemeana na aina ya ngozi uliyonayo, aina ya sita inatengeneza 'melanin' nyingi na uwezo wake ni mkubwa katika kujilinda na madhara ya jua yatokanayo na mionzi," anasema Dk. Kenene.

Anasema mionzi ya jua huleta joto husababisha ngozi kuzeeka haraka, kupasuka kwa midomo ya chini, vipele, chunusi hata kusababisha saratani ya ngozi aina ya melanoma.

Bingwa huyo anasema kadri mtu mweusi anavyokaa katika jua hujikinga zaidi, ikilinganishwa na mtu mweupe.

Anasema watu wenye ulemavu wa ngozi (albino), wana uwezo mdogo wa kuzalisha melanin.

Melanin ni rangi ya kibaolojia, inayopatikana kwenye ngozi, nywele, macho na kuleta tofauti baina ya rangi ya mtu mmoja hadi mwingine, au tofauti kulingana na bara analotokea duniani.

Dk. Kenene anasema mionzi mikali ya jua ina madhara katika ngozi ambayo hujitokeza kwa kipindi cha mwaka mmoja au miwili.

**WENYE CHANGAMOTO**

Dk. Kenene anasema wapo watu waliozaliwa na tatizo kushindwa kuzalisha kinga za kuukinga mwili na miozi ya jua.

Anasema kundi hilo ni la watu wenye ulemavu wa ngozi yaani albino na watu weupe (wazungu).

Dk. Kenene anasema kundi hilo lina hatari ya kupata saratani ya ngozi.

Bingwa huyo anasema kundi lingine linaloathiriwa zaidi na mionzi ya jua ni ambao kwa waliozaliwa na tatizo ni XP, ambao wengi wao hufikishwa hospitalini wakiwa na tatizo la ngozi likiwa kubwa.

"Kundi hili la Xeroderma Pigmentosum (XP) ni jeni za urithi huzuia mwili kurekebisha seli zilizoharibiwa na miale. Sio kwamba ngozi yao haizalishi melanin, hawana uwezo wa kurekebisha uharibifu uliotokana na jua".

**MAGONJWA**

Dk. Kenene anasema kuwa ngozi hupata magonjwa mbalimbali ikiwamo chunusi na mzio ambao ni pumu ya ngozi.

"Kuna madhara yanaonekana hata kwa haraka zaidi kutokana na joto, watoto hutokwa na vipele vidogovidogo au watoto wenye utapiamlo wanakumbana na vipele,"

Anabainisha kuwa saratani ya ngozi hufanya ngozi kuwa na mabaka meusi kama mkaa ambayo baadae hugeuka vidonda.

Anafafanua kwamba watu wazima walio na umri wa kuanzia mika 50 wanaugua ugonjwa huo, ambao huanzia kwenye unyayo wa mguu.

"Ukuiona mabadiliko ya rangi mbili katika mwili inaweza kuwa 'melanoma', ili kuthibitisha tunachukua sampuli kidogo ya ngozi na kupeleka maabara na kusubiri majibu," anasema Dk. Kenene.

**NGOZI NYEUSI**

Wataalamu wa masuala ya ngozi pia wanasema sababu ya ngozi kuwa nyeusi zaidi hutokana na mazingira anapoishi mtu.

Kwamba mtu anayeishi jirani na mstari wa Ikweta kuliko na jua zaidi kwa kipindi cha msimu mzima wa mwaka hasa kwa nchi za Afrika, Asia, Amerika Kusini na Mashariki ya Kati, ngozi huwa nyeusi zaidi.

Inaelezwa kwa takribani miaka 100,000 iliyopita rangi ilianza kubadilika kutoka katika rangi nyeusi sana ya ngozi, na kadri watu walivyoanza kusambaa duniani kote iligundulika kuna maeneo yaliyo na jua kali zaidi na kwingine jua hafifu.

**FAIDA NGOZI NYEUSI**

Walio na ngozi nyeusi huwa wanazeeka taratibu ngozi zao, ikilinganishwa na ngozi ya mtu mweupe.

Kutokana na kwamba kadri binadamu anavyozidi kuwa mtu mzima ngozi inazidi kuwa nyembamba na kuwa rahisi kuharibika kutokana na mionzi ya jua ambayo kwa kiwango kikubwa huhatarisha ugonjwa wa saratani ya ngozi.

Pia ngozi nyeusi hujikinga na magonjwa yanayotokana na jua ikilinganishwa na watu weupe au wenye ulemavu wa ngozi.

**TAKWIMU**

Shirika la Afya Duniani (WHO), linasema takribani watu 132,000 wanaugua saratani aina ya melanoma.

Afrika saratani huua zaidi na kusababisha vifo kwa asilimia 60, huku ikitahadharishwa kwamba ifikapo mwaka 2030, vifo vitafikia asilimia 70, kwa mujibu wa utafiti kuhusu 'Africa's Emerging Cancer Crisis: A

# Kumbe teknolojia ni zana ya kuwapora haki maskini

**Na Mwandishi Wetu**



Teknolojia ya kisasa ya vifaa vya kusaidia upumuaji inayotumia kuhudumia wagonjwa wenye maambukizi ya COVID-19. Mashine hizo na chanjo ni matokeo ya utafiti wa hali ya juu ambao ni nadra kupatikana kwenye nchi maskini. **PICHA: MTANDAO.**

MSINGI mkuu wa haki za binadamu ni kwamba kila mtu anastahili (rights) ambazo kwa kuzaliwa amezipata bila kujali cheo, rangi, taifa, tabaka, jinsia, dini au sababu nyingine yeyote.

Hivyo ni mambo anayostahili kuyafurahia bila kipingamizi wala kuangalia au kurejea chochote kingine, anastahili kuwa nazo kuzifurahia kwa sababu amezaliwa binadamu.

Haki hizi zimeorodheshwa hasa katika Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu lililotolewa na Umoja wa Mataifa (UN) mwaka 1948.

Hoja ya msingi ni kwamba, "watu wote wamezaliwa huru, hadhi na haki zao ni sawa. Wote wamejaliwa akili na dhamiri, hivyo yawapasa watendeane kindugu, wapendane na kuheshimiana bila kubaguana na kuishi kwa upendo.

Kuna haki nyingi zikiwamo za kisiasa ambao ni uhuru wa mawazo, imani, dhamira, kusikilizwa kabla ya kuhukumiwa, kujieleza, kuchanganyika na mkusanyiko.

Haki nyingine ni haki ya kushiriki katika utawala wa nchi pamoja na kushiriki na kupiga kura katika kuchagua viongozi unaosimamiwa na vyombo vilivyo huru na haki , hizo zikiwa ni haki za kisiasa.

Lakini katika haki zote iliyo kuu na ya muhimu ni ya kuishi hivyo watu wanahitaji, uhuru, usalama, usawa wa binadamu, haki ya faragha na kuheshimiwa utu wao na waishi na kufurahia maisha yao.

Lakini dunia ilivyo leo inaelekea kuwa teknolojia inaongeza changamoto za haki za binadamu kwa sababu wasio na teknolojia watazidi kupuuzwa na kuwa na hali duni ikilinganishwa na wale ambao wana fedha, utaalamu na uwezo kiuchumi ambao watakuwa wakizifurahia zaidi haki hizo.

Kuishi ni haki ya msingi kwamba ukizaliwa ukue, uishi, usiuawe wala kupata mateso lakini kuishi mbona hata wanyama nao huishi? Lengo hapa ni kuwa na ulinzi ili uishi na ufurahie maisha lakini kwa jinsi dunia inavyokwenda huenda haki hiyo ya maisha ikaanza kuupuzwa.

Ukiangalia kilichotokea kwenye chanjo ya COVID -19 utaona kuwa wenye fedha kama mataifa ya magharibi ndiyo ambao maisha yao yananusurika kwa kupata chanjo ya maradhi hayo lakini nchi maskini hasa za Afrika hazina uwezo wa kuwekeza kwenye chanjo wala kufanya utafiti wa kupata dawa kwa ajili ya watu wake maskini na kuwachanja ili wasiambukizwe corona.

Hivyo panapotokea magonjwa ya milipuko haki ya kuishi kwa watu maskini inaondoka kwa vile hawana fedha za kutafiti tiba wala kununua dawa kutoka kwenye mataifa yenye teknolojia za kuzalisha dawa hizo na kuwasaidia watu wake.

Hili limethibitika wakati huu ambao mataifa makubwa kama Marekani, Kanada, Uingereza na China yaliwekeza kwenye kuzalisha chanjo na kuchanja baadhi ya raia wake, wakati nchi maskini za Afrika nyingi hazijaamua kuhusu hatma ya kuwachanja watu wake kwa vile hazikuwekeza kwenye utafiti wa kupata dawa hizo.

Idadi kubwa ya maskini duniani ni wale ambao wanaishi katika dunia maskini licha ya kuwa na rasilimali nyingi hasa Afrika Kusini ya Jangwa Sahara, mfano huko ndiko kuna wakulima wadogo, wafugaji, wachimbaji madini na na wamachinga wanaofanya biashara ndogo ndogo.

Hawa ni wale ambao hawana maisha bora, kwa hiyo haki yao ya kuishi ipo lakini si kuishi kama wengine wenye teknolojia ya kisasa.

Haki ya kufanyakazi leo inaelekea itayumbishwa na uwepo wa roboti na binadamu wengi hasa maskini watakosa ajira , mishahara , kiinua mgongo, bima za afya na maisha . Kwa hiyo watabakia kuwa kwenye kundi la walalahoi wasio na ujuzi, utaalamu, mali, elimu bora, fursa tena wanaoishi gizani.

Haki zao pengine za kumiliki rasilimali zao kwa maendeleo zitaondoka kwa vile hawana uwezo wa kuziendeleza kwa sababu hawana teknolojia . Wana dhahabu lakini hawawezi kujiajiri kuichimba wala kuichenjua ili wapate bidhaa zitakazowapa pesa za kuendeleza maisha yao.

Wengine wana madini muhimu kama shaba yanayotumiwa kuzalisha mathalani vifaa vya umeme kama 'motor', nyaya, transfoma' ambayo hutumika kutengeneza mifumo ya umeme kwenye ndege, meli na magari lakini hawana teknolojia ni wazi hatma yao itabakia kuwa shakani.

Afrika ni taifa ambalo linazungumzia zaidi kujichanganya na nchi za magharibi lakini haifikirii ni namna gani itajikomboa kwa kuangalia umuhimu wa kuwa na teknolojia na biashara zake yenyewe kwa maendeleo ya raia wake.

Kwa mfano hadi leo mawasiliano ya simu ni makubwa lakini Afrika inatumia kiasi cha dola pengine milioni 600 kwa mwaka kulipia maunganisho ya mawasiliano ya simu kati ya mabara ya Afrika na Ulaya, lakini hadi leo haijafikiria namna ya kuondoka kwenye utumwa wa kuzilipa Ulaya mabilioni ili kujiunganisha na simu. Wataalmu wako wapi?.

Kumbe kusema kuna haki ya maisha, haki ya maendeleo na haki nyingine lukuki kutabakia kwenye makaburasha iwapo wenye teknolojia wataamua maskini wasio na uwezo wasipate tiba , chakula au mawasiliano kwa kuwa wao ndiyo wanaohodhi na kuwakandamiza maskini ambao wanakosa haki nyingi kwa vile hawana ukwasi.

Kilichotokea kwenye corona kiwe funzo na kihamasishe mataifa maskini kubadilika kwa kuwa hawana namna ya kuwapatia haki raia wake iwapo wako nyuma na wataendelea kulega kwenye teknolojia.

Inawezekana likatokea janga duniani nchi tajiri zikatumia teknolojia kunusuru raia wake lakini Waafrika wakaumia pengine hata kupoteza maisha kwa vile hawana utaalamu wala ujuzi wa kukabiliana na maafa hao.

HABARI KIMATAIFA

# Watu maarufu 30 kushiriki mazishi ya Prince Philip leo

**London,** UINGEREZA

MAZISHI ya mume wa malkia Elizabeth wa Uingereza, Prince Philip, yanafanyika leo na kuhudhuriwa na watu 30 pekee.

Ratiba iliyotolewa na Kasri ya Buckingham, inaonyesha ibada ya mazishi inaanza saa tisa alasiri, ikiwa ni majira ya saa 11 jioni kwa Afrika Mashariki.

Watoto wanne wa Mwanamfalme Philip (99) na Mtawala wa Edinburgh, watalisindikiza jeneza la baba yao katika shughuli ya ibada ya mazishi hayo.

Wanamfalme Charles, Andrew, Edward dada yao Bintimfalme Anne, pamoja na wajukuu wa Malkia, Wanamfalme William na Harry, watatembea pembezoni mwa gari aina ya Land Rover ambalo litaubeba mwili wa Mwanamfalme Philip kuelekea katika kanisa la Mtakatifu George katika kasri ya Windsor.

Wageni wote watavalia barakoa na watakaa umbali wa mita moja kama inavyoelekezwa katika muongozo wa kudhibiti virusi vya corona.

Hata hivyo, Malkia Elizabeth II atakaa ndani ya hema la peke yake.

Watu wote 30 watakaoshiriki ni ndugu wa karibu wa Malkia Elizabeth na mumewe Mwanamfalme Philip.

Orodha hiyo ya wageni inaongozwa na Malkia mwenyewe na watoto wake wanne.

Pia watakuwapo wenza wa watoto wa Malkia, mke wa Mwanamfalme Chalres, Camilla Duchess wa Cornwall, mume wa Bintimfalme Anne, Timothy Laurence na mke wa Mwanamfalme Edward Sophie Countess wa Wessex.

Wengine ni wajukuu wa Malkia na Mwanamfalme Philip wakiongozwa na Mwanamfalme William pamoja na mkewe Kate Duchess wa Cambridge, Mwanamfalme Harry.

Wengine ni, Bintimfalme Beatrice na mumewe Edoardo Mapelli Mozzi, Bintimfalme Eugenie na mumewe Jack Brooksbank, Peter Phillips, Zara Tindall na mumewe Mike Tindall, Lady Louise Windsor na Viscount Severn.

Kadhalika ndugu wa karibu wa familia hiyo wakiwamo watoto wa aliyekuwa mdogo wake Malkia Bintimfalme Margaret; Earl wa Snowdon, Lady Sarah Chatto na mumewe Daniel Chatto.

Ndugu wengine ni Mtawala wa Gloucester, Mtawala wa Kent, Bintimfalme Alexandra na Countess Mountbatten wa Burma.

Ndugu wa Mwanamfalme Philip kutoka Ujerumani ambao watahudhuria ni Bernhard, Mwanamfalme wa Baden, Mwanamfalme Donatus wa Hesse na Mwanamfalme Philipp wa Hohenlohe-Langenburg.

Mwanamfalme Philip alifariki Aprili 9, mwaka huu

**BBC**



Malkia wa Uingereza, Elizabeth II, akiwa na marehemu mumewe, Mwanamfalme Philip, wakati wa uhai wake, akisimama kwa dakika moja mwanzoni mwa sherehe ya bustani huko Buckingham Palace, Mei 23, mwaka 2017 kwa heshima ya wale waliouawa kwenye tamasha la Ariana Grande huko Manchester. **PICHA : BBC**

# Raul Castro kuachia ngazi

**Havana,** CUBA

RAIS wa Cuba, Raul Castro, ambaye ni mdogo wake aliyekuwa kiongozi wa taifa hilo, Fidel Castro, atang'atuka madarakani.

Juzi kongamano la Chama cha Kikomunisti lilifunguliwa ambalo baadae litasitisha miongo sita ya utawala wa Castro na kuachia uongozi kizazi kipya.

Cuba kwa miaka mingi ilikuwa chini ya Fidel Castro ambaye alifariki mwaka 2016, hata hivyo kustaafu kwa Raul, ambaye hivi karibuni atatimiza umri wa miaka 90, alimkabidhi kijiti cha uongozi Rais Miguel Diaz-Canel ( 60).

"Raul hatakuwa kiongozi wa chama tena, lakini ikiwa kuna tatizo Raul atakuwapo, hajafa", Ramon Blande, mwanaharakati wa kikomunisti, 84, alisema.

Miguel Diaz-Canel ambaye bado ni kijana, anakabiliwa na matatizo mbalimbali.

Wajumbe zaidi ya 100 wa chama kimoja, kutoka majimbo yote, watakutana kwa siku nne katika mji mkuu wenye vikao mbalimbali, kujadili maswala makubwa ya nchi.

Uteuzi wa Diaz-Canel kama katibu mpya wa kwanza, wadhifa muhimu zaidi nchini Cuba, unatarajiwa kufanyika siku ya mwisho, Jumatatu.

## Rais Buhari arejea Nigeria baada ya kutibiwa Uingereza

**Lagos,** NIGERIA

RAIS wa Nigeria, amerejea nchini mwake baada ya ziara ya matibabu Uingereza.

Rais wa Nigeria Muhammadu Buhari alikuwa London, alikokuwa akipatiwa matibabu.

Kurudi kwake siku ya juzi kulitangazwa kupitia ujumbe wa akaunti ya Twitter ya serikali.

Rais huyo ambaye alifanya ziara ya kawaida ya matibabu kwenda Uingereza Machi 30, mwaka huu, amekosolewa sana kwa kuamua kutibiwa nje ya nchi

Huku ikidaiwa mfumo wa huduma ya afya nchini mwake ukisimamiwa vibaya na kukosa ufadhili wa kutosha vyombo vya habari vya huko viliripoti.

Nigeria pia inakabiliwa na ukosefu wa usalama, huku mashambulizi kadhaa yakiripotiwa wakati Rais Buhari alipokuwa hayupo.

**BBC**

## Wasichana 100 Chibok hawajulikani waliko

**Lagos,** NIGERIA

OFISI ya Rais wa Nigeria, imeapa kuwaokoa wasichana wa zamani wa shule 112 wanaosadikiwa kubaki katika mikono ya kundi la Boko Haram, tangu walipotekwa nyara kutoka mji wa Chibok miaka saba iliyopita.

Wakosoaji wanashutumu serikali kwa kutofanya vya kutosha kuokoa wasichana hao ambao sasa ni wanawake au kuboresha usalama wa shule.

Taarifa iliyopewa jina la "Wasichana wa Chibok Bado wako akilini mwetu" ilitolewa na ofisi ya rais, juzi, wakati Nigeria inaadhimisha miaka saba tangu wasichana wa shule 276 kutekwa kutoka kwenye shule ya serikali huko Chibok, katika jimbo la Borno.

Mamlaka ilisisitiza wito wake wa kuwatafuta na kuwakomboa wasichana hao 112 waliobaki kifungoni. Wazazi na watetezi wanashutumu serikali kwa uzembe na kutoa ahadi hewa.

Allen Manase ni mkuu wa vyombo vya habari na utangazaji wa jamii ya Chibok.

Karibu wasichana 503 walikuwa shuleni hapo usiku wa kutekwa nyara na Boko Haram, Aprili mwaka 2014.

Kati ya wasichana 276 waliochukuliwa, zaidi ya 100 waliachiliwa kupitia mazungumzo, wakati wengine walifanikiwa kutoroka.

Wiki hii, katika kuadhimisha miaka saba tangu utekaji nyara wao, wazazi wa wasichana waliobaki walikusanyika shuleni kuombea kurudi kwao salama.

Manase alisema serikali iko kimya zaidi juu ya suala hili lakini inalenga tu katika maadhimisho hayo kutoa taarifa.

Katika miezi ya hivi karibuni, utekaji nyara kadhaa mkubwa wa wanafunzi umetokea kaskazini mwa Nigeria, na kusababisha kufungwa kwa shule.

Ripoti mpya ya Amnesty International ilisema zaidi ya shule 600 kaskazini mwa Nigeria zimefungwa kwa sababu ya ukosefu wa usalama tangu Desemba. Nigeria ina idadi kubwa zaidi ya wanafunzi walioacha shule ulimwenguni kulingana na UNICEF, haswa kwa sababu ya ukosefu wa usalama Kaskazini, ambapo uandikishaji wa shule na kiwango cha kusoma ni kidogo sana.

Wakati wazazi wengi wanaendelea kungojea na kutumaini, mawakili na Amnesty International wanasisitiza mamlaka kuzifanya shule ziwe salama.

**VOA**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MNADA**, HARBOR MICROFINANCE CO. LTD AND J&J RECOVERY wanauza nyumba iliyopo kijiji cha Mwandege/Chatembo, Mkuranga yenye hati ya mauziano ya serikali ya mtaa mali ya Obonyo Seda. Mnada ni kuanzia tarehe 19 April, 2021 na kuendelea. Namba za mawasiliano ni 0714292260/0784076588.

## VIWANJA NA MASHAMBA

**GARI INAUZWA,** HARBOR MICROFINANCE CO. LTD AND J&J RECOVERY wanauza gari TOYOTA RAV 4 SHORT CHASES namba T 235 ALJ. Namba za mawasiliano 0714292260/0784076588.

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MAGAMBO KUYI MADUHU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S4157-0025** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **MWAKALUBA** mwaka 2017, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa **DOD/DOD/RB/829741/2020**

## KUPOTELEWA KWA KADI YA GARI

**J.X. BETTING (T) LTD**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Toyota Kluger yenye Na. za usajili **T429DPZ** Chassis Na. **ACU 250008757,** Engine Na. **2AZ0391529** kwa yeyote atkayeiona atoe taarifa kituo cha Poisi kilichokaribu

TAARIFA YA POLISI

**MWA/NY/RB/191255/2021**

## KUPOTELEWA KWA KADI YA GARI

**CATHERINE SHAURI ZENGO**

Anatangaza kupotelewa na Kadi ya grai aina **TOYOTA VITZ** yenye Na. za usajili T488CUB, Chassis Na. **SCP905024830,** Engine Na. **2SZEAA4830** kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.

TAARIFA POLISI

**MWA/NY/RB/191261/2021**

---

**IJAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MBEYA**

**MAOMBI MADOGO NO. 2/2021**

**JOSEPH CHIVILE NA WENGINE 7.........WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**LUMOCONS CO.LTD..........MJIBU MAOMBI**

**MAJALIWA MWAMAKULA..........MJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

Ndugu Majaliwa Mwamakula(MjibuMaombi)unataarifiwa na Mahakama hii, kuhudhuria hapa Mahakama ya Wilaya ya Mbeya au Wakuli wako mnamo tarehe 05/05/2021 siku ya Jumatano saa 2.30 asubuhi ambapo Shauri limepangwa kwa ajili ya kutajwa.
ELEWA KWAMBA, ukikosa siku hiyo, shauri litasilikilizwa bila wewe kuwepo na uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Muhuri wa Mahakama leo hii tarehe 12 Mwezi 04 2021

HAKIMU MKAZI
DISTRICT RESIDENT MAGISTRATE

**HAKIMU MKAZI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DOMINIC MWEMEZI RWEYENDERA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **MUITSUBISHI FUSO** yenye namba za usajili **T 240 DTU** ,chasis namba **FKSIG,** engine namba 5D, yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa

**DSM/PHQ/RB/188802/2021**

## KUPOTEA KWA CHETI



**RAMADHANI JUMA anatangaza** kupotelewa na CHETI na TRANSCRIPT cha chuo cha DODOMA kozi ya BA (SOCIOLOGY) chenye namba za **usajili BA(SO)0001014** kilichotolewa mwaka 2011,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisi taarifa OB/RB/19037/2015**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya DODOMA.**

**Kituo cha DODOMA Mkoa DODOMA.**

**Usimamizi wa mirathi Na 94/2021.**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU CHARLES JONSON MTOWA WA IMAGE**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA GRACE CHARLES MTOWA**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na Mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 03 mwezi 05 mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 14 mwezi 04 mwaka 2021.

---

**IN THE RESIDENT MAGISTRATES' COURT OF ARUSHA AT ARUSHA**

**CIVIL CASE NO. 2 OF 2021**

**ANTONY JOSEPH MENGI................PLAINTIFF**

**VERSUS**

**SAMWEL ROBERT MBISE................DEFENDANT**

**NOTICE OF DATE OF HEARING/MENTION**

***(Rule 13 subordinate courts (Civil Procedures, Summoned & Plaintiff rules, 1955 G.N. No. 292/87) Cap. 2 Sup. 34)***

**TO: SAMWEL ROBERT MBISE – ARUSHA**

**TAKE NOTICE** that the hearing of the above suit has been set down for 6 the MAY at 8:30 am you must produce on that day all the witnesses upon whose evidence and the entire document upon which you intend to reply in support of your case.

***GIVEN under my hand and the seal of the court this 15 day of APRIL, 2021.***

RESIDENT MAGISTRATES
ARUSHA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Baruapepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaawa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA
16/04/2021

**TANGAZO**

Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya J**UMATATU tarehe 19/04/2021**. Kampuni ya **ZAKHEM CONSTRUCTION (T) LIMITED** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **DODOMA** kupitia **VIGWAZA.** Gari hilo lenye namba za usajili na vipimo vya:
**T 892 BPK / T 485 BPF**

**UREFU 23........UPANA 4.3........KIMO 5.2**

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza***

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**Notice of Date of Hearing**

**Civil Appeal/Revision**

**Katika Mahakama ya Wilaya MBARALI katika Wilaya**

**Shauri la Rufaa/Masahihisho Na 16............. 2020**

**Mahakama ya mwanzo ya IGURUSI**

**Daawa Na 39.....................ya 2020......**

**FREDY ADOLPH.....................Mwombaji Rufaa/Masahihisho**

**Mdai/Mdaiwa wa mwanzo .**

**SALIMU TWAAH ..............Mjibu rufaa/Masahihisho Mdai /Mdaiwa wa mwanzo**

**Kwa............ SALIMU TWAAH**

Fahamu kwamba Rufaa /Masahihisho itasikilizwa katika Mahakama hii saa 2;00 asubuhi /mchana ya tarehe 22/04/2021
Hati hii imetolewa kwa Amri ya Mahakama hii leo tarehe 31/03/2021.

HAKIMU MKAZI MFAWIDHI
WILAYA YA MBEYA

## KUPOTEA KWA CHETI



**MANENO BULUNJA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S 2323.0025** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary MHANDE mwaka 2014,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi **DSM/PHQ/RB/191144/2021**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**WINIFRIDA ATHANASE KATEKSI** ANATANGAZA KUPOTEZA KADI YA GARI AINA YA SUBARU FORESTER LENYE NAMBA ZA USAJILI T176 DRB, INJINI NAMBA **EJ20C036665 NA CHESISI NAMBA SG5054652.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI AU YEYOTE SIMU NAMBA 0623217544. AMETOA TAARIFA POLISI NA KUPEWA NAMBA **KAG/BUK/RB/189522/2021**

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**SIMON SAVIO MAKUMBI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA YA USAJILI **T 371 BJZ RANGE ROVER** CHASIS NO: **SALLPAMM3VA370737 ENGINE NO: JAA1007559** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI TAARIFA YA POLISI: **ARU/ARU/RB/190887/2021**

## KUPOTEA KWA HATI YA NYUMBA.

**GRACE CHARLES MTOWA** anatangaza kupotelewa na hati ya nyumba plot Na.25, kitalu 24 Majengo Relini yenye jina la **CHARLES JONSON MTOWA.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DO/RB/7612/2021.**

## MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA LTD, SEPCO DEBT COLLECTION & AUCTIONEERING CO. LTD** tutauza kwa mnada wa hadhara gari la mdhamini wa mdaiwa Sugu **(Abdiel Alphonce Mshana),** Mali ya Ndugu **HAJI IDD MOHAMED (T 777 DBN- TOYOTA NOAH).** Gari lipo katika yard ya Makumbusho.

Lengo ni kufidia/ kupunguza deni la mkopo analodaiwa. Mnada utafanyika **Tarehe 30/04/2021,** mahali dhamana ilipo. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga: 0715683777/0712670704/0713052578**
**Email: info@sepcoauctioneering.co.tz**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HADITHI

# HADITHI

MWANZONI ilionekana ni fahari. Wazazi kupata mtoto wa kike. Akaja kuwa msichana mzuri aliyeumbwa akaumbika na kutamaniwa na kila mtu, ni sifa kubwa. Wakati mwingine mzazi hupata hata vizawadi vidogo kutoka kwa watu mbalimbali bila kujua kuwa nia ni kutengeneza mazingira kwa binti yao. Kinyume chake mzee Ngoma na mkewe Fatuma wanapata mtoto wa kike Bishada ambaye anaondokea kuwa tishio kwenye kijiji cha Mtakuja kwa urembo wake.

Badala ya kuwa tija na faraha kwa wazazi wake anageuka kuwa balaa. Wazazi wanakuwa hawana amani kutokana na vitisho mbalimbali ikiwemo kuuawa kutoka kwa watu mbalimbali ndani na nje ya kijiji hicho. Inakuwa tafrani. Kijiji hakikaliki. watu wanatafutana. Moto unawaka. Bishada mwenyewe maisha yake yanakuwa hatarini. Fuatilia kisa hiki ambacho kitakuacha mdomo wazi.

# Aolewe au afe-2

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

Licha ya sifa zote hizo, hakuwahi kuwa na kiburi au maringo. Aliongea na kucheka na mtu yoyote yule. Wakati mwingine hii iliwafanya baadhi ya wavulana kuona kama vile wako karibuni kukubaliwa.

Akiwa anapika. Bishada bado alikuwa anafikiria jinsi gani atakavyoikataa barua iliyoletwa kwa ajili ya posa.

Hakujua hasa ni nani huyo ambaye alionyesha nia ya kutaka kumuoa. Anachojua wavulana na hata watu wazima tu wengi wameonyesha nia ya kutaka kumuoa. Yeye hakuwa tayari.

Hakuna sababu yoyote ambayo inamfanya afikirie hivyo. Basi tu alidhani muda wake wa kuolewa haujafika.

“Kuolewa ni majaliwa. Kama kuolewa nitaolewa. Lakini siyo sasa hivi. Kwanza jamani ni mpaka mwenyewe umpende mtu mwenyewe anayekuoa?” Alijiuliza mwenyewe, halafu akajijibu. “Yaani uende tu kwa mtu ambaye hata hujampenda, eti kwa sababu tu umeolewa. Mi mbona mpaka sasa sijaona yoyote hapa ambaye nampenda na anaweza kunioa.” Alijiambia mwenyewe huku akionja chumvi kwenye wali aliokuwa anapika.

Aliwaza pia jinsi kikao cha kesho kitakachokuwa cha moto. Kitendo cha kukataa aliona kitawakasirisha wazazi wake, pamoja na wajomba zake.

“Hata kama wananipiga basi, lakini nitawapasha.” Wakati anaongea hivyo alisikia mlango ukigongwa.

Alikuwa na baba yake mzee Ngoma. “Bishada yupo chumbani kwake, au jikoni.” Alisikia sauti ya baba yake ikiuliza.

“Yupo jikoni.” Mama yake alijibu.

Wakati akitarajia kuwa ataitwa, alisikia viatu vikimjongea jikoni. Mzee Ngoma aliingia jikoni pamoja na moshi mwingi, lakini alijitoka ndani.

“Mwanangu Bishada. Kesho jioni tuna kikao. Hicho kikao kinakuhusu wewe. Maongezi yote utayakuta hapo kwa hiyo nakusuhi usiwe mbali. nadhani mama yako amekudokeza kidogo.” Sauti ya mzee Nanga ilikuwa dhahiri masikioni mwa Bishada.

Hakutaka kujibu chochote ambacho kingezua mjadala, au kuweka taswira ya knini kitakwenda kutokea kwenye kikao cha kesho.




“Sawa baba nimekusikia.” Alijibu kwa kifupi, lakini akiwa na mawazo mengi kichwani mwake.

******************************

“Unamfahamu huyu kijana?”

“Nani?”

“Nani unatuuliza sisi tena?”

“Ndiyo maana nauliza, maana simjui.”

“Humjui?”

“Ndiyo.”

Kila mtu alishusha pumzi kwenye kikao hicho. Walichoamini kuwa mpaka barua ile inaletwa ina maana huenda Bishada na mwenzake walishakutana na kumuahidi kuwa ataleta barua kwao.

“Lakini shemeji, hatra kama hamjui na hawajawahi kuonana, lakini ndiyo barua imeshakuja hivyo. Kuna mtu anataka kuoa, je wewe Bishada umemkubali?” Aliuliza Mauya, ambaye ni mjomba wake Bishada.

“Samahani sana wazazi wangu, mjomba na wengineo.” Bishada alisema na kuwafanya walio kwenye kikao hicho kumtegea sikio. Ilionekana kabisa kuna kitu kiliho moyoni mwake anataka kukiongea.

“Mimi huyo mwanaume Duma namfahamu. Anaishi kijiji cha pili kutoka hapa. Ila hatujawahi hata siku moja kukutana na kupanga mipango yoyote. Wazee wangu kuolewa hi hiari. Hata kama nisingekuwa nimewahi kumuona, kama ningekuwa niko tayari kuolewa ningekubali tu. Lakini kwa sasa siko radhi. Kuolewa kwa sasa mimi bado.” Bishada alikuwa akiongea kwa utulivu, lakini kwa uhakika uliochanganyika na aibu akiangalia chini muda wote huo.

“Bado vipi? Wewe umri wa kuolewa tayari. Umeshamaliza kidato cha nne. Baba yako sikuweza kukuendeleza. Sasa watu wanajitokeza kukusitiri unakataa. Unataka kuniletea watoto wasio na baba hapa?” Mzee Ngoma aliongea ingawa kwa sauti ya chini, lakini ilikuwa ua ukali kidogo.

“Baba Bishada, mtoto kakwambia kuwa yeye bado hajajisikia kutaka kuolewa, wewe unataka kumlazimisha. Huwezi kujua, huenda hampendi huyo mwanaume.” Ilikuwa sauti na mama Bishada, Bi Fatuma alimtetea binti yake.

“Unasikia shemeji” Mauya alikohoa kidogo kuliweka koo lake sawa.

“Mimi nadhani itakuwa ni makosa makubwa kumlazimisha binti kuolewa. Ndoa ni maridhiano wa hiari kwa watu wawili. Mmoja anapolazimishwa, au kushurutishwa hiyo siyo ndoa. Na hata kama ikifungwa inakuwa ni batili. Ni kwamba lazima wote wawili waridhie. Tusimlazimishe mtoto. Shemeji na dada, mimi nawaambia hapa kuwa ipo siku akimpata anayempenda, mtaona wenyewe barua inaletwa haraka haraka na yeye atalazimishwa isomwe haraka.”

Kwa maneno hayo ya shemeji yake. mzee Ngoma alitulia na kukubalia kurudisha majibu kuwa mchumba amekataa, barua imekataliwa.

*********************************

Ni mwezi mmoja umepita. nyumbani kwa kina Bishada sasa ilikuwa kama posta. Barua zilizidi kumiminika kutaka kumuoa msichana huyo mwenye haiba ya kupendeza. Kama kawaida alikataa na kuzidi kumkasirisha baba mtu.

**Sikatai kwamba unanipenda na siyo wewe tu. Wengi wanaNipenda na wameleta barua nyumbani, lakini mimi sitaki. Sijaamua kuolewa.**

Mama Bishada yeye alikuwa pande mbili. Akiwa na mumewe alimtetea binti yake na kumwambia ipo siku akimpata anayempenda atakubali. Akiwa na binti yake anamshutumu kwa kosa la kukataa kuolewa.

Mama anajua binti yake ni mzuri. Ana wasiwasi asije akazeekea nyumbani. Uzuri wa msichana ni kama maua. Yanachanua asubuhi na kunyauka jioni.

Siku moja akiwa kisimani muda wa jioni, Duma alipita na kumuona Bishada.

“Enhee bora nimekuona. We Bishada kwa nini umenitia aibu mimi na ndugu zangu, umekataa mimi nisikuoe?”

“Uliniambia kama wewe unaleta barua kwetu?” Bishada alijibu.

“Siyo lazima, mimi nilikuona siku moja ukiwa na shoga zako, nikatokea kukupenda, nikauliza jina na unakoishi wakaelekezwa ndiyo nikaleta barua kwenu.”

“Utaletaje barua kwetu kabla ya kuiona mimi kwanza, halafu ndiyo nikakwambia lete au usilete?”

“Kwa hiyo hilo ndiyo kosa langu?”

“Ndiyo, labda mimi nina mchumba mwingine je?”

“Kwa hiyo nianze upya? Mimi nimekupenda nilete barua kwenu?”

“Si umeleta umekataliwa. We hujui kukataliwa?”

“Sasa Bishada, mimi mwenzako nimekufa kwako, nakupenda sana wewe.”

“Sikatai kwamba unanipenda na siyo wewe tu. Wengi wananipenda na wameleta barua nyumbani, lakini mimi sitaki. Sijaamua kuolewa.” Bishada alimkatisha tamaa Duma.

Hakuwa na la kuongea. Alionekana kuwa na mawazo, hasira, vyote vikichanganyikana na aibu.

“Haya, poa tu, lakini ipo siku tu.”

“Lo, umechelewa babu.” Bishada alijibu kwa nyodo.

Ukweli ni kwamba Bishada hakuwa na mchumba yoyote. Hakuwa na mpenzi yoyote. Bado aliamini kuwa ana nafasi ya kutulia kuliko kufanya papara ya kuolewa.

Njiani alikutana na kijana mwingine anaitwa Mtoka. Yeye pia alikuwa ni mmoja wa walioleta barua hivi karibuni na kupigwa chini.

“Kumbe Bishada umenitakalia mimi, halafu unamkubali Duma. Wewe mtoto wa kijiji cha pili atakusaidia nini badala ya kutukubali sisi wa kijiji hiki hiki?”

“Hivi wewe una akili kweli?” Alimuuliza kwa hasira.

**ITANEDELEA JUMAMOSI**

## HABARI MICHEZO

# AUBAMEYANG APONA, ATOKA HOSPITALI




**LONDON,** England

NAHODHA wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang "anajisikia vizuri" baada kurejea nyumbani akitoka hospitali alikokuwa amelazwa kwa siku mbili kwa sababu ya kuugua malaria, meneja Mikel Arteta amethibitisha.

Starika huyo wa Gabon hakuwa kwenye kikosi cha Arsenal katika michezo yao miwili ya mwisho na alieleza kupitia mitandao ya kijamii siku ya Alhamisi kwamba alipata maambukizi ya virusi ugonjwa huo wakati wa mapumziko ya michezo ya kimataifa.

Aubameyang aliweka picha yake akiwa hospitali kitandani huku akiwa amevaa gauni, lakini kwa sasa ameruhusiwa na afya yake imeimarika.

Akiongea katika mkutano wa habari baada ya ushindi wa Arsenal 4-0 dhidi ya Slavia Prague siku ya Alhamisi na kuona wakifanikiwa kwenda hatua ya nusu fainali kwa jumla ya mabao 5-1 Arteta alisema: "Tumeongea naye, yupo nyumbani sasa, na anaendelea poa.

"Alikuwa kwa siku mbili hospitali kwa ajili ya kupata matibabu sahihi, lakini anajihisi vizuri sasa.

Aubameyang hajaifungia Arsenal tangu alipofunga katika sare ya 1-1 dhidi ya Burnley mwezi Machi 6, mwaka huu katika mechi ya Ligi Kuu England na amefunga mbao 14 kwenye mashindano yote msimu huu.

# Flick kumrithi Low Ujerumani

**MUNICH,** Ujerumani

KOCHA wa Bayern Munich, Hans Flick, anatarajiwa kuondoka klabuni hapo na kujiunga na Timu ya Taifa ya Ujerumani huku akirithi mikoba ya Joachim Low katika kikosi hicho.

Akiwa na Bayern Munich, Flick alifanikiwa kuchukua makombe sita kwa kipindi cha miezi 18 tu.

Flick ataondoka klabuni hapo akiwa na kumbukumbu mbaya ya kushindwa kutetea taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu baada ya kuondolewa na PSG.


Kocha huyo atachukua nafasi ya Low ambaye ameomba kuacha kazi ya kufundisha Ujerumani baada ya mashindano ya EURO 2020.

Ujerumani imekuwa ikiwaajiri makocha wazawa kufanya kazi hiyo na kwa kiwango kikubwa makocha hao huwa wanafanya kazi kubwa sana.

Joachim Low alichukua timu ya ujerumani kwa muda wa miaka 15 na akafanikiwa kuchukua makombe akiwa na Ujerumani, miongoni mwa makombe aliyochukua ni Kombe la Dunia la mwaka 2014 kule Brazil.

Kuondoka kwa Low katika timu ya taifa kunahusishwa na kuchukua nafasi ya Kocha wa Real Madrid, Zinedine Zidane endapo atashindwa kuchukua ubingwa wa UEFA au La Liga.






# Barca wakaribia kumnasa Garcia

**BARCELONA,** Hispania

KLABU ya Barcelona inadai ina uhakika itakamilisha suala la kunasa saini ya Eric Garcia kabla ya mwisho wa mwezi huu.

Mkataba wa Garcia pale Manchester City unafika tamati mwisho wa Juni, na amekuwa akitarajiwa kuwa atarejea Camp Nou kama mchezaji huru licha ya Arsenal na PSG pia kuonyesha nia ya kumsajili.

Ripoti zinadai kuwa mpaka sasa, nyota huyo mwenye umri wa miaka 20 bado hajafanya makubaliano na Barcelona, akiwa tayari amecheza mechi 10 kwa City kwa msimu huu.

Hata hivyo, kwa mujibu wa chapisho la Sports, Barcelona wana uhakika kuwa wanaweza kujihakikishia saini ya staa huyu kabla ya kuisha kwa mwezi huu.

Taarifa zinasema kuwa kocha Ronald Koeman na kikosi chake walilazimika kurefusha ofa ya mkataba kwa staa huyu kutokana na hali ya uchumi ya klabu.

Garcia ambaye aliwasili City tangu mwaka 2017, amekuwa akipata muda mchache sana wa kucheza, na inaonekana itakuwa ni uamuzi mgumu sana kwake kusaini mkataba mpya na timu hiyo ya England.

# City yamnyatia Kayky wa Fluminense

**MANCHESTER,** England

RIPOTI zinadai Manchester City wanajipanga kumsajili kinda wa Kibrazil, Kayky kutoka katika klabu ya Fluminense.

Viongozi hao wa Ligi Kuu England wamekuwa wakihusishwa na fowadi huyo tangu mwaka ulipoanza.

Kwa mujibu wa Fabrizo Romano, City sasa wanakaribia kusaini dili yenye thamani ya pauni milioni 8.7

Kayky yupo kwenye matarajio ya kupokea mkataba wa miaka mitano lakini hatotua klabuni mpaka mwaka 2022 majira ya joto.

Kinda huyo wa miaka 17 ni zao la akademi ya klabu ya Fluminense ambayo iliwatoa wachezaji mbalimbali akiwamo mkongwe wa Real Madrid, Marcelo na Fabinho wa Liverpool.

Mshambuliaji huyo chipukizi amekuwa akitajwa kama Neymar ajaye huko Brazil na winga huyo amebarikiwa kipaji kikubwa cha kuuchezea mpira.

Pamoja na Kayky, City pia walisema wanavutiwa kumleta Metinho huko Etihad akitokea Fluminense.

Wawili hao walikuwa sehemu ya kikosi U17 cha Brazil ambacho kilishinda ubingwa mwaka uliopita kwenye michuano ya U17 ya Copa de Brazil.

Mara nyingi amekuwa akicheza upande wa kulia ambako amekuwa akitoka na mpira na kukimbiza mabeki wa timu pinzani na uwezo wake umekuwa ukilinganishwa na Neymar.




# POGBA ASAINI DILI NA AMAZON PRIME




**LONDON,** England

MCHEZAJI wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Paul Pogba amesaini dili na kampuni ya matangazo ya Amazon Prime ambayo itatengeneza historia ya maisha yake.

"Pogmentary" ndio jina la documentary hiyo ambayo inategemewa kuwa hewani mwakani. Documentary hiyo inatarajiwa kuelezea maisha ya Pogba ndani na nje ya uwanja.

Kiongozi wa Amazon Prime amesema wamefurahi sana kufanya kazi na Paul na wanaamini watatoa documentary safi sana kumhusu yeye!

Pogba ambaye amekuwa na wakati mzuri hivi karibuni katika klabu yake ya Manchester United anaamini kutengeneza documentary hiyo kutasaidia watu wengi zaidi kumjua yeye kiundani.

Kiungo huyo alikuwa na mchezo mzuri sana katika mechi ya juzi dhidi ya Tottenham na watu wengi wanaamini kwamba huko kunaweza kuwa kurudi kwa mchezaji huyo kwenye kiwango chake halisi.

Itakumbukwa kuwa Pogba alisajiliwa na Manchester United kutoka Juventus kwa dau la Euro milioni 110, ambao ulikuwa ni usajili uliovunja rekodi nyingi.

# *Chelsea yamweka sokoni Ziyech*

**LONDON,** England

TIMU ya Chelsea imesema ipo mbioni kuwaacha wachezaji watano ili kurahisisha mchakato wa kumsajili beki wa kati wa Sevilla, Julles Kounde.

Miongoni mwa wachezaji hao ni Hakimi Ziyech.

Ziyech alijiunga na Chelsea majira ya joto mwaka jana kwa dau la Euro milioni 37.5 lakini bado hajaonyesha makali yake tangu kipindi hicho.

Tangu ajiunge na Chelsea amefanikiwa kuhusika na magoli si zaidi ya 10 tofauti na matarajio ya wengi.

Thamani ya Ziyechi katika kikosi cha Chelsea haionekani na pengine Thomas Tuchel ameona ni bora amwache nyota huyo raia wa Morocco.

Ziyech amefanikiwa kuanza katika mechi tano tu kati ya 17 za Tuchel, hivyo nafasi yake inaonekana kupungua siku hadi siku.

Nyota wengine wanaotarajiwa kuachwa kwa mabadilishano ni Kepa Arrizabalaga, Tammy Abraham, Tiemoue Bakayoko na Michy Batshuayi.

Kwa upande wa Kepa, ujio wa Mendy umemfanya awe kipa namba mbili wa Chelsea moja kwa moja.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SOLSKJAER APANIA KUCHUKUA EUROPA

**Asema uwezo kwa kushinda kombe hilo wanao endapo wachezaji wake wataendelea kuonyesha...**

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amesema anatamani na anaamini timu yake itafika fainali ya Ligi ya Europa na kuchukua kombe hilo.

**United ni miongoni mwa timu nne zilizotinga nusu fainali ya Kombe la Europa, huku wakiwa pamoja na Arsenal kutoka Ligi Kuu England (EPL), Villareal kutoka La Liga na AS Roma inayoshiriki Serie A ya nchini Italia.**

Mabao ya United katika mkondo wa kwanza yaliyofungwa na Marcus Rashford na Edinson Cavani yaliwaandalia mazingira mazuri kusogelea hatua ya nusu fainali.

Mechi ya juzi usiku ilikamilika kwa United kushinda mabao mawili, moja toka kwa Cavani na lingine la kujifunga la Vallejo na kufanya jumla ya mabao 4-0.

United watakutana na AS Roma katika nusu fainali ya michuano hiyo itakayochezwa Aprili 29, mwaka huu.

Mechi hii inakumbusha mechi ya mwisho ambapo timu hizi zilikutana mwaka 2007 na Manchester United kuibuka na ushindi wa jumla ya magoli 8-3 kwa mikondo yote miwili ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Katika mechi hiyo pia Solskjaer alikuwa miongoni wa wachezaji walioisaidia United.

Katika mechi hizo mbili, United walianza kupoteza 2-1 wakiwa ugenini, lakini walipofika Old Trafford wakapindua matokeo na kushinda magoli 7-1.

Hii pia ilikuwa ndo mechi iliyomtambulisha Ronaldo kufunga kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya ambaye alifunga magoli mawili.

"Leo tumecheza vizuri sana, na kwa nidhamu kubwa. Tuna nafasi ya kufika fainali na ni lazima tufanye hivyo. Nimeona kila mchezaji anatamani hilo na tutafika fainali licha ya kukutana na timu kubwa," alisema Ole.

## ZISIKUPITE

### POCHETTINO AMTAKA KANE

KOCHA wa PSG, Mauricio Pochettino, amewasiliana na mshambuliaji nyota wa Tottenham na England, Harry Kane, 27, kuhusu uwezekano wa kuhamia Ufaransa. ***(Telefoot on Twitter)***

### KLOPP ANUKIA BAYERN

KLABU ya Bayern Munich itajaribu kumsajili Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp, mwishoni mwa msimu huu, kwa sababu Hansi Flick ataenda kuitumikia Timu ya Taifa ya Ujerumani. ***(90mins)***

### BAYERN: FLICK HAONDOKI

RAIS wa Bayern, Herbert Hainer, anaamini Hansi Flick ataendelea kusalia katika klabu hiyo inayokipiga katika uwanja wa Allianz Arena, licha ya kuhusishwa na kikosi cha Ujerumani. ***(Sky Sport Germany, via Goal)***

### MOURINHO AMWITA FELLAINI

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho anapanga kumsajili kiungo wa Ubelgiji, Marouane Fellaini, 33, ambaye pia alikuwa chini yake kule Manchester United. Fellaini kwa sasa yupo na klabu ya Shandong Luneng ya China tangu Februari 2019.

### SOUMARE SOKONI

KLABU ya Leicester City ipo mbele ya Manchester United katika mbio za kutaka kumsajili kiungo wa klabu ya Lille, Boubakary Soumare, 22. ***(Star)***

### TORRES AGEUKA LULU

MANCHESTER United wanamtaka "kwa udi na uvumba" beki wa klabu ya Villarreal na Hispania, Pau Torres (24), ambaye pia anawaniwa na vigogo wengine wa soka barani Ulaya, Bayern Munich na Real Madrid. ***(AS, via Team Talk)***

### DYBALA HAKIELEWEKI

MAZUNGUMZO baina ya Juventus na mshambuliaji wake, Paulo Dybala (27), ambaye anahusishwa na mipango ya kutaka kuhamia Manchester United bado hayajakamilika kutokana na hali ya kifedha ya klabu hiyo ya Turin, kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Ufundi, Fabio Paratici. ***(Sky Italia, via Goal)***

### CAVANI MAMBO MAGUMU

DAU la pauni milioni mbili kwenye mkataba wa mshambuliaji, Edinson Cavani (34), linaweza kuwa shubiri katika mipango ya mchezji huyo kuihama Manchester United mwishoni mwa msimu. Cavani amekuwa akihusishwa na mipango ya kuhamia Boca Juniors. ***(Mirror)***

### LINGARD ATAJWA ARSENAL

ARSENAL inapanga kuipiku West Ham kwenye kumsajili kiungo wa Manchester United na England, Jesse Lingard, 28, kipindi kinachokuja cha majira ya joto. ***(Star)***

### LIVERPOOL NA PEDRI

LIVERPOOL wanatakiwa kumsajili haraka kiungo wa Barcelona, Pedri, 18, kabla hajasaini mkataba mpya utakaoongeza fedha nyingi kwenye kipengele cha kumuuza. ***(Star)***

# Chikwende aiona Simba ikiyoyoma

**Na Saada Akida**

KIUNGO wa kimataifa wa Simba, Perfect Chikwende, amesema kikosi chao kina ubora wa hali ya juu na bado hajaona timu ambayo itawazuia katika mbio za kusaka ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Chikwende (pichani chini) aliliambia gazeti hili kila mchezaji wa Simba amekuwa akijituma kuanzia mazoezini atakapopata nafasi ya kupangwa kwa sababu ya kutaka kuona wanafikia malengo.

"Nina uhakika msimu huu tunachukua tena ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania, kwa sababu kila mchezaji hapa kambini akili na nguvu zetu ni kufanya vizuri katika michezo iliyopo mbele yetu,".

"Hatutakuwa tayari kupoteza pointi yoyote hivyo nina imani ubingwa ni wetu kwa sababu hadi sasa hatujaona timu ambayo itatuzuia katika kukamilisha mipango yetu," alisema Chikwende.

Nyota huyo alisema anaomba mashabiki wa timu hiyo kuendelea kuisapoti timu yao kama wanavyofanya sasa kwa sababu wachezaji wanapambana kufikia malengo ya kutetea taji wanalolishikilia.

Naye Mtaalamu wa takwimu wa timu hiyo, Calvin Mahvunga, alisema kwa sasa nguvu kubwa wameelekeza katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara kwa sababu wanataka kukaa kileleni na kupunguza presha katika michezo ijayo ya kimataifa itakayofuata.

Mahvunga alisema ana imani na kikosi cha timu hiyo kuwa kitaendelea kuvuna pointi katika kila mchezo watakaocheza hasa mechi za viporo ambazo zinawakabili.

Alisema hana wasiwasi wala mashaka kuhusu nafasi yao ya kutwaa ubingwa kutokana na kutambua umuhimu wa kushinda taji hilo kwa mara nyingine.

"Nikiiangalia Simba naiona mbali sana, natamani kuiona klabu hii ikiwa inafanana na moja ya klabu kubwa kama Mamelodi Sundowns (Afrika Kusini) au Al Ahly ya Misri," Mahvunga alisema.

Aliongeza timu zote kubwa duniani zimekuwa na wakufunzi wengi katika kila idara na hii hupelekea kila kiongozi katika benchi la ufundi kufanya kazi kwa weledi wa hali ya juu na kuendelea kufanya vyema katika mashindano mbalimbali.



# WAZIRI AAHIDI KODI VIFAA VYA MICHEZO KUPUNGUA

**Na Saada Akida**

NAIBU Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Paulina Gekul, amesema wanajipanga kuhakikisha kodi kwa vifaa vya michezo inapungua ili wafadhili wengi watoe misaada mbalimbali ya vifaa hivyo kwa wanamichezo hapa nchini.

**Gekul alitoa kauli hiyo baada ya kupokea viatu jozi 120 vilivyokabidhiwa kwa Serikali kwa ajili ya kukipatia Chama cha Riadha (RT), kutoka katika Kampuni ya JICA ya Japan.**

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Gekul alisema anaamini riadha pamoja na michezo mingine inapaswa kuungwa mkono na wadau mbalimbali ili kufikia maendeleo.

Gekul alisema kupunguzwa kwa kodi ya vifaa vya michezo kutasaidia baadhi ya vyama vya michezo vilivyojenga uhusiano mzuri na kampuni nyingine kupata misaada ya vifaa kama ilivyo kwa JICA.

"Serikali inatambua suala la michezo ni ajira, kazi na afya basi tutasimamia na kutekeleza yale yote ikiwamo kutatua changamoto wanazozipata vyama vya michezo ili kuendeleza michezo kwa taifa letu," alisema Gekul.

Kiongozi huyo alitoa rai kwa RT kuhakikisha vifaa vilivyotolewa vinakwenda kwa watu sahihi pamoja na kushirikiana vyema na JICA kuandaa mashindano mengine nje ya jiji la Dar es Salaam.

"Nina imani mikoani kuna wachezaji wazuri lakini hawafikiwi, hivyo naomba Chama cha Riadha na wengine kwenda huko kutafuta vipaji kwa ajili ya kuandaa timu bora ya Taifa hapo baadaye," alisema Naibu Waziri huyo.

Aliongeza serikali itaendelea kushirikana bega kwa bega na RT katika kuiandaa timu ya Taifa iliyoko kambini jijini Arusha inayojiandaa na Michezo ya Olimpiki itakayofanyika nchini Japan baadaye mwaka huu.

Wakati huo huo, Gekul alifungua mafunzo kwa watu wenye ulemavu na amewataka viongozi wa vyama vya michezo kutumia vizuri mafunzo wanayopata kuhusu utawala bora pamoja na kuweka wazi matumizi ya fedha.

"Baada ya mafunzo haya mtaibua vipaji kwa watu wenye ulemavu pamoja na timu zenu kufanya vizuri katika michuano mbalimbali," alisema Gekul.




Naibu Waziri katika Wizara ya Habari Utamaduni, Sanaa na Michezo, Paulina Gekul (katikati), akipokea vifaa vya michezo kutoka kwa mwakilishi wa Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (JICA), Yamamura Naofumi, kwa niaba ya watu wenye ulemavu jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Naibu Katibu Mkuu wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Neema Msita. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Namungo FC yalia na uchovu

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya timu yake kuchapwa mabao 2-1 na Polisi Tanzania, Kocha Mkuu wa Namungo FC, Hemed Morocco (pichani), amesema kucheza mechi nyingi za kimataifa kumesababisha wachezaji wake kuwa na uchovu na kushindwa kufanya vyema katika Ligi Kuu Bara.



Akizungumza baada ya mechi yake ya 'kiporo' iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa Ushirika mjini Moshi mkoani Kilimanjaro, Morocco alisema wachezaji wake hawakucheza vizuri kabisa katika mechi hiyo na hasa kipindi cha kwanza.

"Hiki ni kipindi cha mpito. Kuna aina fulani ya uchovu kwa wachezaji wangu kwa sababu ya kucheza mechi nyingi mfululizo. Kama unavyojua tunakabiliwa na mechi za kimataifa na za Ligi Kuu, zote zimekuwa karibu karibu na wakati mwingine kusafiri. Hii inasababisha wachezaji kuchoka na kutocheza kwa viwango vyao vya kawaida," alisema Morocco.

Kocha huyo alisema kipindi cha kwanza walifanya makosa mengi ambayo ilibidi waadhibiwe zaidi, lakini angalau kipindi cha pili walipunguza makosa na kutengeneza nafasi ambayo moja wapo walipata bao la kufutia machozi.

"Hatuwezi kulaumu kipa, beki, au washambuliaji. Sisi tukipoteza, tunapoteza timu nzima na tukishinda, tunashinda timu nzima, wala hatuna haja ya kuangalia nani nakosea na nani kapatia," alisema kocha huyo.

Kichapo hicho kinaiweka Namungo inayoshiriki mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika katika nafasi ya 12 kwenye msimamo wa ligi ikiwa na pointi 28 baada ya kucheza michezo 20 wakati Yanga yenye pointi 51 ikiendelea kukaa kileleni.

Michezo

Jumamosi Aprili 17, 2021

Nipashe



Solskjaer apania kuchukua Europa UKURASA 22




Mabeki wa Yanga, Lamine Moro (kushoto), na Bakari Mwamnyeto, wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Biashara United itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. **PICHA: SAADA AKIDA**

# Yanga, Biashara mechi ya kibabe

**Na Adam Fungamwango**

MBIO za kuwania ufalme wa soka nchini zinatarajia kuendelea tena leo kwa vinara, Yanga kuwakaribisha Biashara United kutoka Musoma mkoani Mara katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Vinara hao watakuwa wanasaka ushindi wao wa kwanza tangu Februari 20, mwaka huu walipoichapa Mtibwa Sugar bao 1-0 , kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa na baada ya hapo hali ilianza kuwa tete kwa kukubali kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Coastal Union na kufuatiwa na sare nyingine ya bao 1-1 dhidi ya Polisi Tanzania.

Jumamosi iliyopita Yanga ilikubali tena kulazimishwa sare nyingine ya bao 1-1 dhidi ya KMC FC na kuwaruhusu watani zao ambao wana viporo vitatu kuwakaribia katika msimamo wa ligi, baada ya kuwa nyuma kwa pointi mbili.

Akizungumza na gazeti hili jana jijini, Kocha Mkuu wa Yanga, Juma Mwambusi, alisema wameshasahau matokeo yote ya mechi za nyuma na sasa wanaangalia ya mbele na kikubwa wamefanya marekebisho katika kikosi hicho, hivyo leo watakuwa na mabadiliko.

Mwambusi alisema wachezaji wake wameimarika na sasa kikosi kimekamilika baada ya majeruhi na waliokuwa wanatumikia adhabu ya kadi kurejea.

"Mechi ya kesho (leo), itakuwa na mabadiliko, tumeona wapi tulikuwa tunafeli na kwa nini tulikuwa hatutumii nafasi ambazo tulikuwa tunazipata. Tumeyafanyia kazi, wachezaji wameelewa na wapo tayari kupambana," alisema Mwambusi.

Alisema wanaiheshimu Biashara United kwa sababu ni moja kati ya timu bora kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na katika msimamo wa ligi hiyo ipo kwenye nafasi za juu, lakini wao kama Yanga wana faida ya kucheza uwanja wa nyumbani.

# SERIKALI YAINGILIA KATI SAKATA LA SIMBA, FCC

## Mbivu, mbichi kujulikana keshokutwa, Ndugai apigilia msumari...

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

SERIKALI imesema vikwazo vilivyoibuka katika uwekezaji wa mfanyabiashara, Mohamed Dewji, maarufu Mo, katika Klabu ya Simba vinatarajiwa kumalizika keshokutwa wakati Tume ya Ushindani (FCC), itakapokutana kwa mara ya tatu na pande zinazohusika.

Kauli hiyo imetolewa bungeni jijini Dodoma jana na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa, baada ya kutokea mjadala mkali kuhusu suala hilo.

Mjadala huo uliibuliwa na Mbunge wa Mlalo mkoani Tanga, Rashid Shangazi (CCM), kushika shilingi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, akiitaka serikali kumaliza ukiritimba kwenye uwekezaji nchini, akiutolea mfano uwekezaji wa Mo katika klabu hiyo kongwe nchini.

Shangazi alisema hakuna sheria maalum inayoongoza uwekezaji katika Sekta ya Michezo, bali sheria inayotumika ni ya Baraza la Michezo (BMT) ambayo alidai ina upungufu.

Baada ya kujenga hoja yake hiyo huku akishangiliwa na baadhi ya wabunge, Shangazi alihoji ni lini serikali itawasilisha bungeni sheria hiyo na kumaliza mvutano wa kiuwekezaji unaoendelea ndani ya Simba.

Katika majibu yake, Waziri wa Nchi, Ofisi nya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Geofrey Mwambe alisema : "Kilichotokea ni kwamba, zilikwenda kampuni nne na mwekezaji mmoja na baada ya hapo Tume ya Ushindani (FCC) iliona kuna upungufu katika mchakato mzima.

"Serikali inafuatilia kwa karibu kuona mgogoro huo unakwisha kwa manufaa ya maendeleo ya michezo na uwekezaji nchini."

Licha ya majibu hayo, Shangazi alisimama na kusema wanachokilia wabunge ni Sera ya Uwekezaji ambayo itakuja kuondoa ukiritimba huo huku akiendelea kushika shilingi ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Ndipo akasimama Waziri Bashungwa, ambaye alisema iko fursa kubwa ya uwekezaji katika Sekta ya Michezo na Sheria Na. 18(a) inabainisha wazi kwamba mtu anawekeza kuwekeza kwenye timu ya michezo kwa kiwango kisichozidi asilimia 49 ya hisa na hicho ndicho kilichozingatiwa katika uwekezaji kwenye Klabu ya Simba.

Alisema FCC na Simba watakutana kwa mara ya tatu Jumatatu ijayo, yaani keshokutwa na serikali inaamini huo ndiyo utakuwa mwisho wa mvutano wa kiuwekezaji ndani ya klabu hiyo.

Spika Ndugai akilizungumzia suala hilo, alisema wanataka limalizwe haraka, akisisitiza: "Haiwezekani klabu kubwa inayojiandaa kwa hatua ya nusu fainali ya Klabu Bingwa Afrika kukwamishwa kwa jambo dogo ambalo limechukua miaka mingi. Tunataka limalizwe haraka na wenzetu wa upande wa pili wajifunze."

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >